# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumamosi Mei 25, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579927

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Madiwani wataka mwongozo sheria kwa malipo ya korosho

UKURASA 3







UKURASA 13

# Sirro amhakikishia usalama Tundu Lissu

UKURASA 2




IGP Sirro

Tundu Lisu

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MFUMO SASA KUDHIBITI VIVUKO KUJAZA ABIRIA**

SERIKALI inatarajia kufunga mfumo maalumu wa kutoa taarifa kwenye...

UKURASA WA 3

**MAKANDARASI WOTE NCHINI KUHAKIKIWA**

KUTOKANA na kukithiri kwa malalamiko ya kukwama kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kama ya maji...

UKURASA WA 7

**WAZIRI AWASHA UMEME KWA BABU WA KIKOMBE**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, jana aliwasha umeme katika Kijiji cha Samungena Digodigo...

## Mbunge Chadema aingia matatani

**NI** kutokana na kauli yake kuhusu Stiegler's Gorge, agoma kufuta kauli, apewa siku tano kuthibitisha...*Endelea Uk. 2*

## Wakaguzi plastiki wapewa masharti

UKURASA 2

**MICHEZO** SEVILLA: SIMBA NI HATARI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

## Mwongozo kwa wakaguzi mifuko plastiki

**Romana Mallya**

OFISI ya Makamu wa Rais, imetoa mwongozo kwa wakaguzi na watekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki kwa halmashauri zote ambapo imeelekeza maeneo yatakayokaguliwa ni pamoja na maduka makubwa ya bidhaa (super market), magengeni na sokoni.

Pia mwongozo huo umetaka ukaguzi ufanyike kwenye maduka ya kawaida, ghalani, viwandani na kwingineko na kusisitiza kuwa wakaguzi hawaruhusiwi kumsimamisha mtu na kumpekua au kupekua mizigo yake ili kutafuta mifuko ya plastiki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na ofisi hiyo, wakati wote wakaguzi wametakiwa wajitambulishe na kuonyesha vitambulisho vyao kwa wahusika kwenye maeneo watakayokagua.

"Hairuhusiwi kuingia kwenye makazi ya watu au kusimamisha magari au vyombo vingine vya usafiri ili kutafuta mifuko ya plastiki," imeagiza.

Pia taarifa hiyo ilisema kuwa iwapo magari au vyombo vingine vya usafiri vitasimamishwa kwa sababu nyinginezo na kukutwa na shehena ya mifuko ya plastiki, adhabu stahiki itatolewa kwa mujibu wa sheria na wahusika wataelekezwa mahala mahsusi kwa kupeleka shehena hiyo.

"Atakayekutwa na kosa la kuendelea kuuza, kuhifadhi au kutumia mifuko ya plastiki ataekelezwa pa kuipeleka mifuko hiyo, atapigwa faini inayostahiki kwa mujibu wa Sheria na atasainishwa fomu kukubali faini hiyo.

Pia ilisema muhusika atapewa muda wa kuilipa faini kama Sheria inavyoelekeza na atakapokataa kusaini au kushindwa kulipa katika muda uliopewa, atafunguliwa mashtaka.

"Watakaotozwa na kulipa faini watapewa risiti za serikali kwa malipo hayo. Busara itumike katika utekelezaji wa katazo hili na matumizi ya nguvu ikiwamo kuwapiga au kuwabeba na kuwaweka ndani watu, hayataruhusiwa.

Pia taarifa hiyo ilisema: "Watakaokaidi au kutotoa ushirikiano katika ukaguzi au kuzuia au kuhujumu utekelezaji wa Sheria au kuendelea kufanya makosa baada ya kuelekezwa au kupewa adhabu, watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali zaidi kwa mujibu wa sheria nyingine za nchi."

# Sirro amhakikishia Tundu Lissu ulinzi

**Na Enock Charles**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, amemhakikishia Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, usalama wa kutosha atakaporejea nchini akitokea kwenye matibabu nchini ubelgiji.

Kamanda Sirro amesema kurejea kwa Lissu kutasaidia kukamilisha uchunguzi na kufahamu waliohusika na shambulio lake.

Akizungumza na Nipashe jana, Sirro alisema kama raia wengine wa Tanzania, anahakikishiwa usalama wake kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

"Kwanza tunashukuru kuwa amepona na sasa anarejea... tutaweza kufahamu zaidi waliohusika na shambulio dhidi yake, lakini pili usalama wake ni jambo la muhimu kama raia mwingine yeyote wa nchi hii," alisema na kuongeza: "Ndio maana hata wewe upo salama, kwa hiyo tutahakikisha anakuwa salama."

Jumatano, mbunge huyo kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), alitaja tarehe rasmi ya kurejea nchini kuwa ni Septemba 7, mwaka huu.

Lissu ambaye kwa sasa anatembea kwa msaada wa gongo moja, amepanga kurejea siku hiyo tarehe ambayo mwaka 2017, alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana.

Septemba 7, mwaka juzi, Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi akiwa ndani ya gari nyumbani kwake Area 'D' jijini Dodoma na watu hao wakati akitoka bungeni.

Akizungumza na gazeti hili Jumatano, Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Vijana wa Chadema (Bavicha), Patrick Ole Sosopi, alisema Mwenyekiti wa Taifa wa Chadema, Freeman Mbowe, aliwapa taarifa kuwa Lissu amemwambia kuwa atawasili nchini tarehe hiyo.

"Tuliambiwa na mwenyekiti wetu kuwa Lissu amesema atarejea Tanzania Septemba 7, mwaka huu na atakuwapo kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa," alisema.

Katika ukurasa wa Bavicha Instagram, waliandika: "Lissu atawasili nchini Septemba 7, mwaka huu na mapokezi yake yatatangazwa kitaifa."

Awali taarifa za kurudi kwa mbunge huyo zilianza kusambaa kupitia video fupi ikumuonyesha Mbowe akiwataarifu wanachama wa chama hicho kuhusu kurejea kwa Lissu.

Baada ya shambulio hilo la risasi, Lissu ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Upinzani Tanzania alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Dodoma kwa matibabu ya awali na siku hiyo hiyo usiku alihamishiwa katika hospitali moja mjini Nairobi, Kenya.

Lissu ambaye pia ni Mwanasheria Mkuu wa Chadema, alikaa siku 121 hospitali ya Kenya hadi Januari 6, mwaka jana, alipohamishiwa hospitali nyingine nchini Ubelgiji ambako Desemba 31, alimaliza matibabu yake ya awali na kuanza ziara nchi mbalimbali.

Januari 19, mwaka huu, Lissu alihojiwa katika kipindi cha Dira ya Dunia cha Idhaa ya Kiswahili ya BBC na kuonyesha nia ya kugombea urais mwaka 2020 kama wanachama na viongozi wenzake wa Chadema watampa ridhaa hiyo.

Januari 21, Lissu alihojiwa kwenye kipindi cha HardTalk kwenye Televisheni ya BBC na mtangazaji maarufu Stephen Sackur, kipindi ambacho kilizua mjadala mkubwa kutokana na namna alivyojibu maswali.

Februari 20, mwaka huu, Lissu alifanyiwa upasuaji wa 23 wa mwisho kwenye goti la mguu wa kulia katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Leuven, Gasthuisberg nchini Ubelgiji, na alisema baada ya hapo atarejea Tanzania.



Rais John Magufuli, akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa O.R. Tambo, nchini Afrika Kusini jana, kuhudhuria Sherehe za Uapisho wa Rais Mteule wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa, ambaye anatarajiwa kuapishwa leo. **PICHA: IKULU**

# Mbunge matatani Stiegler's Gorge

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Catherine Ruge (Chadema), ameingia matatani bungeni baada ya kupinga utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa umeme katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge.

Jana, wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka ujao wa fedha, Ruge alijikuta akitakiwa kuwasilisha ushahidi kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge baada ya kupinga mradi huo na serikali kudai kwamba hoja zake hazina ukweli.

Ruge, alisema Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauona mradi wa Stiegler's Gorge kama diwani ya 'Songs of Lawino and Okol', akisisitiza kuwa Watanzania wanapaswa kutambua una madhara na hautawanufaisha.

"Stiegler's Gorge si mradi unaoelezeka, na namwomba Mungu waheshimiwa wabunge turudi hapa 2020 ili mthibitishe maneno yangu," alisema.

Ruge alisema gharama za utekelezaji wake hazielezeki huku akinukuu taarifa ya msomi aitwaye Jorge Hitman, ambaye alisema utatekelezwa kwa gharama ya Sh. trilioni 21 wakati serikali ikieleza kuwa utagharimu takribani Sh. trilioni 10.

Aliendelea kulieleza Bunge kuwa, kwa kuwa benki ambazo zimefuatwa kushiriki utekelezaji wa mradi huo hazina uwezo, anaona haitakuwa rahisi utekelezaji wa mradi huo kufanywa kwa kutegemea mapato ya ndani.

Aliongeza utekelezaji wa mradi huo pia utaathiri watu zaidi ya 500,000 wanaoishi pembezoni mwa Bonde la Mto Rufiji na Hifadhi ya Selous.

**USHAHIDI**

Wakati Ruge anaendelea kuwasilisha mchango wake bungeni, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisimama na kuomba kutoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayoelekeza kuwa mbunge hatatoa bungeni taarifa yoyote ya uongo.

Mgalu alisema Ruge ametoa taarifa ya uongo wakati anachangia kuhusu Stieger's Gorge kwa kuwa mradi huo ulifanyiwa tathimini, tenda ilitangazwa na wakandarasi

INAENDELEA UK. 8



Wanafunzi wakitembea bila ya kuvaa viatu kwenye maji machafu yaliyotuama katika sehemu ya Barabara ya Nkrumah, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya zao. **PICHA: JOHN BADI**

# Madiwani wataka mwongozo wa kuibana serikali korosho

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wametaka mwongozo wa kufungua madai ya kuishinikiza serikali kulipa fedha za korosho kwa msimu wa mwaka 2018/19.

Waliwasilisha mwongozo huo jana kwa mwanasheria wa halmashauri hiyo, Joshua Sanga, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani.

Kadhalika, walimtaka Mkuu wa wilaya hiyo, Selemani Mzee, kutoa kauli ya kuwahakikishia ni lini wakulima hao watalipwa.

Kwa mujibu wa madiwani hao, wakulima hawajui ni lini watalipwa fedha zao na madiwani wanakosa majibu ya uhakika kwenye mikutano ya maendeleo ya kata (WDC), na kwamba wanashangazwa kutotekelezwa kwa ahadi ya serikali.

Walisema pamoja na ahadi ya serikali kuwa watalipa wenye chini ya kilo 1,500, hadi sasa kwenye kata zao kuna kundi la wakulima wenye chini ya kilo hizo na zaidi ambao hawajalipwa.

Diwani wa Lipumbulu, Jemsi Chigoo, alisema mwanasheria wa Halmashauri hiyo anapaswa kutoa muongozo wa kisheria kwa madiwani wote ambao wakulima wao hawajalipwa malipo ya korosho uwasaidie kufungua madai mahakamani dhidi ya serikali.

Walisema kesi hiyo itapunguza au kuondoa maswali mengi wanayoulizwa na wananchi na wanakosa majibu ya moja kwa moja.

"Kila wanapokwenda kuangalia fedha zao benki kwenye akaunti zao hawakuti chochote, hali ambayo imewakatisha tamaa na kuamua kurudi kwa madiwani wao, ili kuomba

INAENDELEA UK. 8

## Sababu makandarasi wote kuhakikiwa

**Na Mary Geofrey**

KUTOKANA na kukithiri kwa malalamiko ya kukwama kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kama ya maji na barabara, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imeanzisha operesheni ya kuwahakiki makandarasi wote waliosajiliwa nchini.

Uhakiki huo utakaofanyika kwa miezi sita maeneo yote nchini wakiwamo makandarasi wa ndani na nje ya nchi, utaenda sambamba na kuwafutia usajili na kushusha madaraja kwa wale wanakaokutwa wamekiuka taratibu na sheria za bodi hiyo.

Msajili wa CRB, Rhoben Nkori, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uhakiki huo utakaoanza kuanzia Jumatatu.

"Kumekuwapo na malalamiko kwa baadhi ya makandarasi kufanya kazi chini ya kiwango, hasa tumekuwa tukipigiwa simu za malalamiko kwenye miradi ya maji kusuasua, ujenzi wa barabara na ujenzi wa zahanati. Hivyo tumeamua kuanzisha operesheni maalum ambayo

INAENDELEA UK. 8

## Mfumo sasa kudhibiti vivuko kujaza abiria

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI inatarajia kufunga mfumo maalumu wa kutoa taarifa kwenye vivuko vyote vinapokuwa vimezidisha kubeba idadi ya abiria na mizigo, lengo kuu ni kupunguza matukio ya ajali.

Mfumo huo pia utaweza kumwonesha nahodha wa kivuko endapo anasinzia au kufanya makosa ambayo yanaweza kusababisha kutokea kwa ajali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi), Elias Mwakalinga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Kongamano la pili la mafundi sanifu, lililokuwa na kauli mbiu 'Wajibu wa mafundi sanifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini'.

Mwakalinga alisema kazi ya kufunga mfumo huo itaanza mwaka ujao wa fedha, ambapo kivuko kikizidisha kubeba idadi ya abiria

INAENDELEA UK. 8


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Peter Naniyo Phissoo | Kiwanja | Mfugoni- Mdobwa Msata | 22/06/2019 | Tausi A/Mart |
| Zaituni Rashid Shaha | Kiwanja | Kijij Cha Kiwangwa | 08/06/2019 | Tausi A/Mart |
| Veronica Waziri Lugongo | Kiwanja/ Nyumba | Bago - Kiwangwa | 08/06/2019 | Tausi A/Mart |
| Sylvia Yohana Sikwaze | Plot | Bago - Kiwangwa | 08/06/2019 | Tausi A/Mart |
| Hamis M.Kazumba /Mariam Madenge | T348 AZN - Chaser | Makumbusho Yard | 31/05/2019 | Champion A/Mart |
| Zainabu Hussein Njovu | Kiwanja | Mgeninani-Mbagala kuu | 15/06/2019 | Tausi A/Mart |
| James Paul Kitonga | Nyumba | Kivule- Kitunda | 08/06/2019 | Champion A/Mart |
| Jared Joel Swabi | Nyumba | Kichangachui-Vingunguti | 04/06/2019 | Champion A/Mart |
| Abiud Alphonce Zagwi | Nyumba | Mji Mpya -Kipawa | 15/06/2019 | Champion A/Mart |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**Tausi A/Mart: 0719351040 ;**
**MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).**
**Champion Auctioneer: 0654200448/0756761328**

215247802



UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI

KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI

KINONDONI

MIRATHI NA ...7... YA 2019...

Maombi ya barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu ...DONALD NEHEMIA HANCE

NA

IRENE DONALD HANCE ........WAOMBAJI/MWOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA

[Kanuni ya 75]

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia Mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za Usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe ...6...... Mwezi ...6........ 2019.

Imewasilishwa JUMATANU Leo tarehe 6.. Mwezi ...5............ 2019

..............................

HAKIMU MKAZI

MAHAKAMA YA KIVUKONI/KINONDONI

215247302

# Wabunge walia migogoro hifadhi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kutatua changamoto ya migogoro ya ardhi kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi za taifa.

Wakichangia bungeni jana mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka ujao wa fedha, wabunge hao wamesema migogoro hiyo imekuwa ikikwamisha maendeleo ya wananchi na hifadhi katika maeneo husika.

Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta (CCM), aliipongeza wizara hiyo kwa kazi kubwa iliyoifanya kudhibiti ujangili na kuendeleza utalii nchini, lakini akaitaka ishirikiane na maofisa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwenda Urambo kutatua migogoro ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi.

"Kumekuwa na mgogoro wa mpaka kwa muda mrefu Urambo. Katika miaka ya 2000, nakumbuka mwaka 2007, serikali ilirasmisha mipaka na kuweka mawe ambayo mpaka sasa yapo.

"Lakini baadaye wizara nayo ikaja na mipaka yake, na bahati mbaya wakachoma nyumba na mali za wananchi wakiwa kwenye mipaka halali. Mpaka sasa hakuna utatuzi wa suala hili. "

Serikali iende ikakae na wananchi, waone wanamalizaje hili.

Mbunge wa Viti Maalum, Josephine Gezabuke (CCM), alisema maeneo ya malisho ya wanyama yamepungua kutokana na ongezeko la watu.

Alisema serikali inapaswa kutenga maeneo mapya kwa kumega kwenye hifadhi kwa ajili ya wafugaji ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (Chadema), aliitaka serikali kupunguza tozo katika hoteli kwa kuwa zimekuwa zikirudisha nyuma jitihada za wafanyabiashara.

Mbilinyi alisema tozo zinazotozwa katika hoteli nchini zimekuwa nyingi, hivyo serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kuziondoa ili kulinda ustawi wa biashara nchini.

Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mahmood Mgimwa (CCM), alisema aliitaka serikali ilieleze Bunge mikakati ya kuendeleza vyura wa Kihansi.

"Vyura wa Kihansi hatusikii kitu chochote, vyura hawa wanazaa. Wenzetu wazungu waliwachukua na sisi tumekaa kimya, ukija waziri utuambie sisi tuna mkakati gani katika kuendeleza vyura hawa," alisema.

Mbunge wa Kaliua, Magdalena Sakaya (CUF), ameitaka serikali kuhakikisha inaongeza nguvu katika kukabiliana na changamoto ya ukataji miti.

Sakaya alisema kasi ya ukataji miti nchini inatisha, hivyo kuna haja serikali kuupa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kupewa mamlaka kamili ya kisheria kupambana wakataji wa miti.

Mbunge wa Kilwa Kusini, Vedastus Ngombale (CUF), aliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kudhibiti tembo ambao wamekuwa wakiua watu kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mbunge wa Mtwara Mjini, Maftah Nachuma (CUF), aliitaka serikali kufanyia kazi changamoto ya baadhi ya askari wanaopiga raia baada ya kuwakamata wakiuza mkaa.

Mbunge wa Viti Maalum, Jackline Musongozi (CCM), alitaka wizara hiyo kuwapa motisha askari wa wanyamapori kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na kuuliwa na wanyama wakali na majangili.

# Wamachinga wa Mwenge wasuasua kuhamia Cocacola

**Na Enock Charles**

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu kama 'machinga waliohamishiwa eneo la Cocacola' wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam kupisha upanuzi wa marabara ya Mwenge-Morocco, wamelalamikia ubovu wa miundombinu katika eneo hilo jipya.

Wamachinga hao wamedai kuwa Mwenge lilikuwa eneo lenye mazingira mazuri, hivyo kuiomba Serikali kuwasadia kuboresha miuondombinu .

Wamedai kutokana na ubovu wa miundombinu hiyo, baadhi ya wenzao wameshindwa kuhamia katika eneo hilo jipya, huku wengine wakiendelea kufanya biashara katika eneo la awali. Muuza viatu, Masoud Ally, ameliiomba Serikali kusaidia kuboresha miundombinu katika eneo hilo jipya ili kuwawezesha wafanyabiashara kuendelea na biashara zao badala ya kutumia muda mwingi kujiboreshea miundombinu.

"Kwa sasa bado tupo wachache tokana na ubovu wa miundombinu... wapo wanaokuja kuchungulia na kuweka alama kisha kuondoka, na wengine wanarejea kule kwa mwanzo hasa ikifika jioni," Masoud alisema.

Naye mfanyabiashara wa mitumba, aliyejitambulisha kwa jina la Elias, alisema kutokana na eneo hilo kuwa na viwanda vingi kuliko makazi ya watu, ni changamoto kwao hasa kwa wakati huu ambapo wafanyabiashara wengi hawajahamia rasmi katika eneo hilo.

"Ukiangalia hapa eneo hili limejaa viwanda population (idadi) ya watu ni ndogo, kwa hio ni ngumu kufanya biashara hasa kwa sasa ambapo hatujahamia wote huku, watu bado wanapata huduma kule kwa mwanzo" Elias alisema.

Serikali ilitangaza kuwahamisha wafanyabiashara hao kutoka eneo la Mwenge na kuwapatia eneo jipya la Cocacola ili kupisha upanuzi wa barabara ya Mwenge-Morocco kwa kiwango cha njia nne.

Hata hivyo, kasi ya kuhamia katika eneo hilo jipya ni ndogo kutokana na madai kuwa kuna changamoto ya miundombinu.



Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi nchini (CRB), Rhoben Nkori akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana kuhusu uhakiki wa makandarasi. Habari Uk. 3 **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# TPSF, Ewura, NEEC kujadili ajira za wazawa Stiegler's Gorge

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwekezaji la wananchi Kiuchumi (NEEC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) zimepanga kukutana makandarasi wanaotekeleza mradi wa kufua umeme mto Rufiji ili waweze kutoa fursa za ajira kwa wazawa.

Mkurugenzi wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati taasisi hiyo pamoja na NEEC zikiainisha fursa zitokanazo na uanzishwaji, utekelezaji na ukamilishwaji wa mradi huo unaogharimu dola za kimarekani bilioni 2.9.

Simbeye alisema wameandaa mkutano wa wadau utaofanyika Juni 11, jijini Dar es Salaam lengo likiwa ni kuongeza ufahamu kwenye mradi na fursa zilizopo.

"Mkutano huu utahudhuriwa na makandarasi kutoka Misri wanaoutekeleza mradi huo pamoja na timu ya usimamizi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) wanaousimamia ambao watatoa mawasilisho kwa wadau siku hiyo," alisema.

Alisema matarajio ni pamoja na kuwasikiliza makandarasi hao wa Misri kuhusu mpango wao wa kushirikisha wazawa katika utekelezaji wa mradi huo na kuwapanga watanzania waweze kushiri kikamilifu.

Pia alisema matarajio mengine ni kuwafahamisha Watanzania kuhusu fursa zinazotokana na mradi haswa aina ya vifaa na bidhaa zitakazohitajika kutoka Tanzania.

"Kuwataarifu wafanyabiashara ambao wana hamu ya kushiriki katika minyororo ya thamani mbalimbali na kuwapatia ujuzi pamoja na nyenzo zitakazowawezesha kushiriki kikamilifu kwenye mradi," alisema.

Simbeye alisema majarajio mengine ya mkutano huo ni kuwasikiliza wahusika wa mradi kuhusu utaratibu ambao wazawa wanaweza kushiriki katika zabuni mbalimbali.

Pia alisema jambo lingine ni kufahamu aina ya kampuni na sekta mbalimbali ikiwemo ya watoa huduma wanakaohitajika katika kutekeleza mradi huo wa mabilioni.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa kitengo cha biashara cha Bajaj Auto Ltd kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini, Vishal Gupta (wa pili kulia), akizungumza katika futari iliyoandaliwa na Bajaj-METL iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkuu wa Bajaj-METL, Indrabhuwan Kumar Singh (watatu kushoto), Meneja wa Bajaj –Boxer Tanzania, Swapnil Jain, Balozi wa Bajaj nchini, Japheti Kaseba (wapili kushoto) na Msaidizi wa Mkurugenzi wa Masoko, Sakina Alloo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Janeth Magufuli afunda Waislamu

**Na Romana Mallya**

MKE wa Rais, Janeth Magufuli, amewaomba Waislamu nchini wakati wakiendelea na mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani wasisahau kuliombea taifa.

Mama Magufuli alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi msaada wa vyakula kwa ajili ya futari kwa vikundi mbalimbali vyenye uhitaji.

"Nimeguswa kutoa sadaka zangu kwa watu wenye uhitaji, ninatoa mchele tani tano, sukari tani 3 na tende. Kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kipindi cha toba, ni kipindi cha kutenda matendo mema na kujizuia na vitendo viovu.

Aliongeza: "Hivyo basi ninamuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema azikubali funga za Waislamu wote na kuwalipa malipo stahiki."

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata), Mwalimu Nuhu Mruma, Mkurugenzi wa Hijja wa Bakwata, Sheikh Haidary Kambwile na wawakilishi wa vikundi mbalimbali vya wenye uhitaji.

Mama Magufuli alisema pamoja na kwamba Tanzania kuna watu wenye imani za dini tofauti, wamekuwa wakishirikiana bila ubaguzi nyakati zote za dhiki na raha. "Binafsi nilivyokua mdogo ilikuwa tukitaka kuchinja kukua au mbuzi au ng'ombe tulikuwa tunatafuta muislam atuchinjie, ni kutokana na utamaduni uliojengeka miongoni mwa Watanzania," alisema.

Naye, Katibu Mkuu Bakwata, Mwalimu Mruma, alimshukuru mama Magufuli kwa moyo aliouonyesha kwa waislam ambao wapo kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

# Msomi awapa changamoto viongozi, wahadhiri Afrika

**Na Beatrice Moses**

VIONGOZI na wahadhiri barani Afrika, wametakiwa kujihoji wasomi wanaozalishwa kwenye nchi zao wanatumiwa namna gani katika kuwezesha mataifa yao kupiga hatua za maendeleo.

Akizungumza jana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wakati akitoa mada maalumu kwenye Tamasha la 11 la Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Prof. Patrick Lumumba, kutoka Kenya alisema kuna mengi ya kujihoji.

"Tujiulize tuna wataalam wa afya, wahandisi, wataalamu wa masuala ya sheria, wanatumikaje katika maeneo yao kuleta maendeleo," alisema Prof. Lumumba.

Alitumia nafasi hiyo pia kukosoa baadhi ya viongozi barani Afrika ambao wamekuwa na utamaduni wa kwenda kutibiwa nje ya nchi wanapungua, wakati kuna wataalamu mbalimbali wakiwamo mabingwa wa upasuaji.

Alisema licha ya baadhi ya nchi kusifika kwa kuwa na hospitali kubwa za rufaa,bado viongozi wake hawana imani na madaktari.

"Wanapougua wanakwenda kutibiwa nje kule India licha ya kwamba hawawatambua vyema madaktari wanaowatibu huko, lakini ajabu ni kwamba wanakuwa na amani kuwa wanatibiwa vizuri," alisema.

Alisema hata hivyo, ameona tofauti kidogo tangu Rais John Magufuli aingie madarakani, kuna mabadiliko kwa kuwatumia wasomi wataalamu.

Alikosoa pia Waafrika kuendelea kuyaruhusu mataifa ya kigeni kujinufaisha na rasilimali za bara hili wakitumia mbinu mbalimbali ikiwamo kujenga majengo ya vyuo na viwanja, huku wasomi wa nchi husika wakishindwa kuonyesha uwezo wao kitaaluma.

Profesa Lumumba alisema ni vyema kuendeleza juhudi za kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika ikiwa ni kutimiza ndozo za Kwame Nkurumah ili Waafrika nao waweze kupata cha kujivunia mbele ya mataifa ya kigeni.

Alisema lugha ya Kiswahili ni miongozi mwa zana ambayo inaweza kutumika katika mawasiliano ya Afrika, katika masuala ya biashara na elimu hivyo kuunganisha nguvu ya kuimarisha umoja kama ilivyo kwa nchi za Ulaya zinavyotumia Kingereza.

Alibainisha wageni wameendelea kubuni mbinu za kuendelea kutawala bara la Afrika kwa njia mbalimbali, ikiwamo kuzipangia mambo ya kufanya ikiwamo kusisitiza uwepo wa vyama vingi kama demokrasia.

"Ningepata nafasi ya kuandika barua kwa wanaharakati wa ukombozi wa nchi za Afrika ningewaeleza mengi ikiwamo utitiri wa vyama vya siasa na migogoro inayoendelea, Mwalimu Nyerere ningemwambia CCM bado ipo madarakani na inafanya vizuri licha ya uwepo wa vyama vingi," alisema.

# Siri chui wa Dar yafichuka

**Na Romana Mallya**

KAMBI ya askari wanyamapori iliyowekwa kwa siku saba Goba maeneo ya Zone C maarufu kwa Prof. Msanjila jijini Dar es Salaam, ili kumsaka chui aliyedaiwa kuonekana, imebaini mnyama aliyeleta taharuki ni pakapori ajulikanaye kama Mondo.

Naibu Kamishna Mhifadhi Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (Tawa), Mabula Nyanda, aliliambia Nipashe jana kuwa mnyama waliyemuona ambaye wananchi walimfananisha na chui ni Mondo.

"Mnyama aliyeonekana siyo chui bali ni Mondo, kama mnakumbuka Mei 13 kulikuwa na taarifa kuwa maeneo ya Goba kumeonekana chui, tuliweka mtego na kambi tangu siku hiyo hadi Mei 19 bila mafanikio," alisema.

Alisema baada ya tarehe hiyo askari wanyamapori waliamua kuondoka kutokana

INAENDELEA UK. 8



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ratiba mpya Ligi Kuu Bara isirundike viporo

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2018/ 19 inatarajiwa kumalizika Jumanne.

Siku hiyo timu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika zitashuka uwanjani ili kumaliza msimu huu.

Tayari bingwa wa msimu huu ameshajulikana, ambaye ni Simba ya jijini Dar es Salaam na ikiwa imefanikiwa kuchukua taji hilo kwa mara ya pili mfululizo na kuwaacha watani zao Yanga ambao walikuwa pia kwenye mbio hizo wakishindwa kung'ara.

Hata hivyo, mechi za ligi hiyo siku ya kufunga pazia zitachezwa kwa malengo mawili, moja la kukamilisha ratiba na nyingine ni kupambana ili zisishuke daraja.

Kwa maana hiyo, Simba ataungana na Yanga, Azam FC, Mtibwa Sugar, Lipuli FC, KMC FC, Ndanda FC, Mbeya City, Coastal Union na Alliance FC kucheza mechi ya kukamilisha ratiba, lakini pia zikihitaji kushinda ili kumaliza msimu kwa furaha na vile vile kulinda heshima.

Upande wa pili ni ule wa Jasho na Damu ambao utahusisha klabu za Singida United, Stand United, Mbao FC, Tanzania Prisons, Biashara United, Kagera Sugar, Ruvu Shooting, Mwadui na JKT Tanzania kupambana kusaka pointi ili waweze kusalia katika ligi hiyo.

Timu ya African Lyon yenyewe tayari imeshashuka daraja na itashuka dimbani kukamilisha ratiba ya msimu huu, kutokana na kufanya vibaya.

Nipashe linasema kuwa, kumalizika kwa msimu huu ni ishara sahihi kwamba maandalizi ya msimu ujao yanatakiwa yaanze mapema ili kuondoa sintofahamu wakati msimu huo mpya utakapoanza.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi (TPLB) mnatakiwa kutumia vema muda huu kujipanga hasa kutoa ratiba ambayo itazingatia mazingira halisi ya timu za hapa nchini.

Kumekuwa na kelele mbalimbali kila inapotolewa ratiba ya ligi kwa baadhi ya klabu kuonekana kama zinapendelewa na nyingine zinakandamizwa, hasa pale wanaposafiri kwenda zaidi ya mara moja kwenye mikoa au kanda ambazo zina timu mbili au tatu.

Ratiba imekuwa ikiwaumiza zaidi wachezaji ambao wengi klabu zao huwasafirisha kwa usafiri wa barabara na hivyo hufika kituoni wakiwa wamechoka na kushindwa kuonyesha viwango vya halisi.

Umefika wakati TFF na Bodi ya Ligi mkatoa ratiba ambayo inazingatia kalenda za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho na maandalizi ya Timu ya Taifa ambayo hucheza mechi za kirafiki na za mashindano ili kuepuka mlundikano wa 'viporo'.

Kilichotokea msimu huu kwa Simba ambayo ilifika hatua ya robo fainali katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kuwa na mechi za viporo zaidi ya 10, ilionekana kama vile kuna mpango mkakati wa kutaka kuibeba timu hiyo.


Lakini uhalisia ni kuwa, baada ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa, wachezaji wake walikosa muda wa kupumzika kutokana na kutakiwa kucheza mechi nyingi ndani ya muda mchache.

Gazeti hili linawakumbusha viongozi wenye dhamana ya soka kubadilika kwa kutoa ratiba kama nchi nyingine zinavyotoa na hapo itasaidia kuipa thamani ligi hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Jifanye mnyonge upate kujua



Na Barnabas Maro

**NJIA** nzuri ya kujifunza jambo kutoka kwa mtu mwingine ni kujifanya mnyonge au kutoonyesha kwamba walijua. Methali hii hutumiwa kumshauri mtu mwenye nia ya kuongeza maarifa yake kwamba asione ugumu wa kujifanya mnyonge ili afaidike.

Ufafanuzi huu ni maalum kwa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kuruhusu vilabu vya Ligi Kuu kusajili wachezaji wengi kutoka nchi za nje. Kwani Tanzania haina wachezaji wenye uwezo kama au kuliko wao? Wapo wengi ila tunashindwa namna ya kuwapata na kuwafunza itakiwavyo.

Tunaambiwa "chako ni chako, cha mwenzio si chako." Kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Twafunzwa kuvitegemea vitu vyetu wala sio vya watu wengine.

TFF yapaswa kuanzisha chuo maalum cha mafunzo ya kandanda kwa vijana wanaopenda mchezo huo. Chuo hicho kiwe na walimu wazawa watakaoongozwa na wataalamu wa kandanda watakaoisaidia nchi na hata kutakiwa na vilabu vya viungo kutoka nje ya nchi. Kwa utaratibu huo Tanzania yaweza kupata wachezaji mahiri wa kandanda watakaoisaidia nchi na hata kutakiwa na vilabu vya Ulaya.

Nashindwa kuelewa ni kwa nini TFF imeruhusu vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kusajili wachezaji wa kigeni hadi kumi kwa msimu mmoja.

Nashindwa kuelewa ni kwa nini TFF imeruhusu vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kusajili wachezaji wa kigeni hadi 10 kwa msimu mmoja! Kwa nini isiwe wachezaji wawili au watatu ili kuwapa nafasi wachezaji wetu? Baadhi ya wachezaji wa kigeni hawana tofauti na wachezaji wetu na mara nyingine wachezaji wetu huonekana kuwa bora zaidi ya wageni.

Kupunguza wingi wa wachezaji kutoka nje utawanufaisha wachezaji wetu kwani watapata nafasi ya kucheza nje ya nchi kwa kusajiliwa na vilabu vikubwa vya Uingereza, Ujerumani, Italia, Hispania, Ufaransa n.k. Hii itakuwa manufaa kwa pande zote mbili yaani Tanzania na wachezaji watakaosajiliwa nnje ya nchi.

Tusihadaike na rangi, tamu ya chai ni sukari. Maana yake tusidanganyike kutokana na rangi ya chai kwani utamu wake hutokana na sukari. Methali hii yaweza kutumiwa kumkanya mtu kutopumbazwa au kutovutwa na sifa za nje za kitu ila akichunguze kwa ndani.

Wachezaji wageni wanaocheza kandanda nchini, hasa timu za Azam, Simba na Yanga ni wangapi huitwa makwao kuzichezea timu za mataifa yao? Labda ni wawili tu waliosajiliwa na Simba kutoka Uganda na mmoja kutoka Rwanda ndio huitwa kuzitumikia timu zao za taifa zinaposhiriki michezo ya kimataifa.

Waliobaki huja Tanzania kujitafutia maisha baada ya kushindwa kuzivutia timu za Ulaya na Afrika. Wengine, kama twakumbuka, walijileta wenyewe nchini kutafuta timu za kuwasajili. Iliposhindikana walirejea kwao kimya kimya na njaa zao!

Tanzania imegeuzwa kuwa 'jalala' la kupokea 'makapi' kutoka nnje nasi kuwapapatikia kama afanyavyo kuku anayechinjwa! Kama wangekuwa wa maana wangesajiliwa na vilabu vikubwa vya Afrika na Ulaya kama walivyo kina Mbwana Samatta na wengineo.

Msimu wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara umemalizika kwa Simba Sports Club wanaofahamika pia kama 'Wekundu wa Msimbazi,' kutwaa ubingwa kwa mara ya pili mfululizo. Cha kushangaza ni kuwa imetwaa ubingwa huo ikiwa kwenye mji wa Singida kama ilivyokuwa msimu uliopita!

Tofauti ni jinsi ilivyokuwa msimu uliopita na huu uliomalizika majuzi. Msimu wa mwaka jana, Simba iliutwaa ubingwa wakati wachezaji wake wakiwa hotelini kutokana na Yanga kufungwa 1-0 jijini Mbeya na Tanzania Prisons.

Msimu uliomalizika hivi karibuni, pia Simba ilitwaa ubingwa ikiwa Singida pia kwa kuifunga timu hiyo mabao 2-0 ingawa bao la pili lilikuwa na mushkeli (kasoro). Hata kama lisingekubaliwa, bado Simba ni bingwa kwa bao la awali lililofungwa na mshambuliaji wao hatari, Meddie Kagere mapema kipindi cha kwanza na kukosa majibu ya wenyeji, Singida United.

"Mambo yafaayo watu ni yaingiayo chunguni." Maana yake mambo yanayofaidi watu ni yanayoingia chunguni. Hutumiwa kumtanabahisha mtu kuwa njia nzuri ya kumsaidia mtu aliye shidani ni kumkabidhi kitu sio kumpa ahadi au kumtolea maneno matupu tu.

Viongozi wanapaswa kufahamu kuwa "Ahadi ni deni (na deni ijuzie)." Maana yake ahadi ni kama deni, mtu akitoa ahadi lazima aitimize. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutimiza ahadi tutoazo. Wachezaji wasifanywe kama watoto wadogo wasiojua maana. Viongozi wawe makini kwa ahadi watoazo.

"Dama ni iliyo mkononi." Dama ni aina ya kamba inayotumiwa kufungia tanga la chombo cha baharini. Maana yake dama inayoweza kutumiwa au kumfaa mtu ni aliyo nayo mkononi. Kitu kinachoweza kumfaa mtu ni alichonacho karibu wala sio kilicho mbali.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Andrew Chenge, akichangia jambo katika semina ya mapitio ya Bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2018/2019 iliyofanyika kwenye ukumbi wa Msekwa, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Hasunga akunwa vijana kuchangamkia kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameelezea kufurahishwa na kasi ya vijana nchini kujiunga na kujishughulisha na kilimo tofauti za siku za nyuma ilivyo kuwa vigumu kukuta kundi hilo likishawishika kuingia katika sekta hiyo.

Hasunga aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua Jukwaa la Fikra la Mwananchi, lililofanyika katika ukumbi wa Kisenga, jengo la Milleinum Tower, Dar es Salaam.

Takwimu za mwaka 2014 za Integrated Labour Force Survey chini zinaonyesha kwamba vijana ni asilimia 56 ya nguvu kazi ya taifa, hivyo wakihusishwa na kuwezeshwa ipasavyo kwa kuwavutia kwa kuzingatia mahitaji yao ya msingi katika kuwekeza katika kilimo, watalifikisha taifa katika maendeleo chanya.

Alisema Wizara ya Kilimo ina Mkakati wa Taifa wa Vijana wa kuwawezesha kushiriki katika kilimo kwa kuzingatia malengo makuu 10 yakawemo upatikani wa ardhi, upatikanaji wa mitaji, mafunzo ya ujasiriamali na uhakika wa masoko ya bidhaa zao. "Swali kubwa na msingi hapa ni je, sisi wadau wote kwa ujumla tunayatekeleza haya ili kuwavutia vijana kushiriki uwekezaji katika kilimo kupitia mnyororo wa thamani? Kwani tunakwama wapi?," alihoji Hasunga.

Alisema ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya 2025 ya kufikia uchumi wa kati wa viwanda, kunahitajika kilimo bora kitakachowezesha upatikanaji wa malighafi za kutosha kutumika katika viwanda.

Pia alisema kilimo chenye tija kitawezesha kipato cha wakulima kuongezeka na hivyo kuwezesha wananchi wengi kufikia kipato cha kati. "Nina uhakika ifikapo mwaka 2025 tunaweza kufikia uchumi wa kati na pengine kuzidi kiwango hicho tulichojiwekea na hapo tutaiona Tanzania mpya yenye neema" Alisema

Mhe Hasunga alieleza kuwa Wizara ya Kilimo imeanza kufanya marekebisho ya Sera ya Kilimo na kutunga Sheria ya Kilimo, hatua ambazo zitaimarisha usimamizi na kutoa mwongozo wa maendeleo ya sekta ya kilimo kwa ujumla.

Kongamano hilo la Jukwaa la Fikra au Mwananchi Thought Leadership Forum (MTLF) lilirushwa mubashara na Kituo cha Matangazo cha ITV pamoja na Radio One Sterio likiwa na lengo la kujadili masuala yanayowagusa Watanzania moja kwa moja kwa lengo la kuyatafutia suluhisho kwa pamoja kupitia mijadala iliyotolewa.

Alisema tangu majukwaa ya namna hiyo yalipoanza mwaka 2018 yakihusisha pia IPP Media (ITV, Radio na Capital Radio) masuala kadhaa yamejadiliwa ikiwa pamoja na mada za kuvutia kama vile "Magonjwa Yasiyoambukiza", mada ya "Tanzania ya Viwanda" na masuala ya Mazingira. Kupitia jukwa hili, Mamilioni ya Watanzania wamefaidika kwa kutoa na kusikiliza maoni katika Nyanja hizo kupitia mitandao ya jamii, televisheni, radio na magazeti.

Mhe Hasunga alisisitiza kuwa Serikali haiwezi kufikia malengo yake bila kuwashirikisha wadau, aliwakaribisha wananchi na wadau wote kujadili na kutoa mawazo yatakayo iwezesha

# Waziri awasha umeme kwa Babu wa Kikombe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nishati Dk. Medard Kalemani, jana aliwasha umeme katika Kijiji cha Samungena Digodigo Wilaya ya Ngorongoro kwa kuuzindua rasmi nyumbani kwa Ambilikile Mwasapila maarufu kama 'babu wa kikombe'.

Akizungumza wilayani humo jana wakati wa kuzindua umeme wa mradi wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya tatu, Dk. Kalemani alisema amewasha umeme kwa mara ya kwanza nyumbani kwa babu wa kikombe kama ishara ya kufungua maendeleo mapya wilayani humo.

Alisema babu ni maarufu na alianza kumsikia mwaka 2011 wakati akitoa kikombe, hivyo ameamua kuizindua nyumbani kwake umeme huo kama ishara ya kufungua maendeleo katika Kata ya Samunge na wilaya yote.

"Mimi leo sijaja hapa kwako kunywa kikombe, hapana nimekuja kwa kazi moja tu ya kuwasha umeme,"alisema.

Mbali na kuwasha umeme nyumbani kwa Babu wa Kikombe, pia aliuwasha Kituo cha Afya Digodigo, Shule ya Msingi Bisikene iliyopo Kata ya Digodigo na Ofisi ya Afisa Tarafa Digodigo.

Aidha, aliwaagiza makandarasi wa kampuni ya Nipo Group wahakikishe ndani ya mwezi mmoja wamesambaza umeme huo Kata ya Samunge na Digodigo ili wananchi waitumie fursa hiyo kujipatia maendeleo.

Alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 40 kwa ajili ya umeme, hivyo vema kila mwananchi ahakikishe anawasha nyumbani kwake umeme kabla ya kulazimishwa.

Pia aliagiza makandarasi hao kuajiri vibarua wasiopungua 60 ili kazi niende kwa haraka.

Naye Naibu Waziri wa Elimu,Sayansi na Teknolojia, Willium Ole Nasha, alishukuru Serikali kupeleka umeme Ngorongoro na kuzindua rasmi.

Kwa upande wake Ambilikile Mwasapila (Babu wa Kikombe) alishukuru Serikali kumwashia umeme nyumbani kwake.

Halisema hatua hiyo ni ishara ya kutimia kwa ndoto yake anayoonyeshwa na Mungu kila mara kuwa Tanzania ni kioo cha Afrika. "Sasa hizi ndizo ishara, zimeanza kuonekana," alisema.

# Mji Tabora kuwa na mwonekano mpya

**Na Munir Shemweta,** TABORA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amezindua Mpango Kabambe wa Uendelezaji Mji wa Tabora na kuzitaka mamlaka husika kuhakikisha zinasimamia vyema mpango huo ili kuleta matokeo chanya.

Akizungumza katika uzinduzi huo juzi, Lukuvi alisema kazi kubwa baada ya kuzinduliwa mpango huo ni wahusika kuusimamia kwa kufuata sheria na kuacha tamaa ya kuwasikiliza baadhi ya watu wenye vyeo wanavyotaka wakati wa kutekeleza.

"Utekelezaji wa mpango kabambe niliouzindua leo (juzi) usiangalie vyeo, pesa au ukubwa wa mtu bali ufuate sheria na msipofanya hivyo hamtapanga miji na kazi yote itaharibika" alisema.

Lukuvi aliwataka madiwani kote nchini katika halmashauri zao kutumia vikao kushughulikia masuala ya ardhi ikiwamo utekelezaji mpango kabambe na kuacha kutumia uamuzi binafsi wa viongozi jambo linaloweza kuchangia migogoro ya mara kwa mara.

Lukuvi alisema msingi mkubwa wa uandaaji mpango kabambe ni kuwezesha ardhi yenye miundombinu, uboreshaji huduma za jamii, kuwa na miji iliyopangwa, kuhifadhi mazingira na kusisitiza kuwa miji yote inahitaji mipango kabambe ili kuepuka ujenzi holela.

Kwa mujibu wa Lukuvi, mpango uliozinduliwa katika manispaa ya Tabora utapunguza migogoro ya ardhi na kuchochea utekekezaji wa malengo ya serikali kuekekea uchumi wa kati wa viwanda na kubainisha kuwa hali hiyo inajidhihirisha katika mpango huo ambao asilimia kumi ya ardhi imepangwa kwa matumizi ya viwanda.

Waziri Lukuvi pia alizitaka taasisi mbalimbali zinazotoa huduma katika Manispaa ya Tabora kuzingatia mpango kabambe wakati wa utekekezaji kazi zao na kuacha kuharibu miundombinu kama vile ujenzi wa miundombinu ya maji na kusisitiza kuwa lazima wakati wa ujenzi wake kuwe na matoleo ya njia za maji.

Akizungumzia uendelezaji mji wa Tabora, Lukuvi alisema kutokana na mpango huo, thamani ya maeneo ya mji huo imepanda, hivyo wamiliki wake ni vyema wakaitumia fursa hiyo kujiendeleza kiuchumi.

Hata hivyo, alisema hakuna mwananchi anayemiliki eneo katika mji huo atakayebomolewa nyumba kwa kisingizio cha mpango kabambe bali uendelezaji wowote utakaofanyika ufuate mpango uliopitishwa.

Meya wa Manispaa ya Tabora, Leopard Opodo, alimweleza Waziri Lukuvi kuwa mpango aliouzindua utakuwa dira ya manispaa katika uendelezaji wa sekta mbalimbali kama vile afya, maji, barabara na kusisitiza kuwa utaondoa ujenzi holela katika maeneo mbalimbali ya manispaa hiyo.

# Mfumo sasa kudhibiti vivuko kujaza abiria

INATOKA UK. 3

mlio wa hatari utalia na hakitaweza kuondoka kwenye gati. "Tutaweka mfumo wa kutoa taarifa pindi kunapotokea hatari kwenye kivuko, kama kwenye lifti za maghorofa 'alarm' inalia watu wakizidi, kwa nini tushindwe kuweka kwenye vivuko," alisema Mwakalinga.

Mwakalinga alirejea ajali ya kivuko cha MV.Nyerere iliyotokea Septemba mwaka jana ambapo abiria zaidi ya 200 walifariki, sababu kuu ikielezwa ni kuzidisha abiria.

Kuhusu kongamano hilo, Mwakalinga alisema mafundi sanifu wana mchango mkubwa katika kufanikisha safari ya Tanzania kufikia uchumi wa viwanda.

Alisema idadi ya mafundi sanifu walisajiliwa ni 112, idadi ambayo ni ndogo kulinganisha na wanaohitimu katika vyuo vikuu nchini.

"Natoa wito mafundi sanifu wote wajisajili, Serikali tupo tayari kushirikiana na mafundi sanifu ili kuipeleka fani ya ufundi sanifu juu zaidi," alisema Mwakalinga.

Aliongeza kwa mwaka wa fedha ujao, serikali itaanza kuwajengea uwezo wahandisi wataalamu wazawa kupitia miradi mikubwa inayotekelezwa hapa nchini.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB), Mhandisi Ninatubu Lema, alisema idadi ya wahandisi nchini ni ndogo, ambapo uwiano wa kufanya kazi ni mhandisi mmoja anafanya kazi na mafundi sanifu watano.

# Siri chui wa Dar es Salaam

INATOKA UK. 5

na kumsaka kwa kushirikiana na uongozi wa serikali za mitaa na wananchi karibu maeneo yote bila mafanikio.

"Jumatatu majira ya saa nne usiku tulipigiwa simu tena ikitutaarifu kuwa wamemuona tena chui na safari hii ameonekana maeneo ya wazi mtaa wa Kibululu, Goba," alisema.

Alisema baada taarifa hiyo, askari wanyamapori walikwenda na kuanza msako kwa mara nyingine na safari hiyo walipata mashuhuda watatu ambao waliwaeleza wamemuona.

"Msako ulianza usiku huo huo tulikagua kila sehemu na hatimaye tukafanikiwa kuona nyayoza paka pori ajulikanaye kama Mondo, tulimuona," alisema.

Alisema licha ya kumuona Mondo, wanaendelea na uchunguzi zaidi kwa kuhusisha na maeneo mengine ya jirani. Kuhusu picha ya awali iliyoonekana mitandaoni ikionyesha chui akiwa kwenye makazi ya watu, Nyanda alisema wamefanya uchunguzi na kubaini ilipigwa nchini India na siyo Tanzania.

Awali baada ya taarifa hizo kuzagaa mtandaoni, Nipashe ilipozungumza na Mkurugenzi wa Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Maurus Msuha, alisema walituma askari wao wenye silaha aina ya shotgun kwa ajili ya kumsaka chui huyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyokuwa mtandaoni, iliwataarifu wananchi wa Kibululu kuwa Ofisi ya Serikali ya Mtaa imewataka wachukue tahadhari kwa sababu kuna chui ameonekana maeneo ya Zone C.

"Habari zetu ndugu wajumbe, taarifa kwa wana Kibululu, Ofisi ya Serikali ya Mtaa inapenda kuwataarifu wananchi wote kuwa kuna chui ameonekana maeneo ya Zone C Kwa Prof. Msanjila, hivyo tuwe na tahadhari wakati tunawasubiri mamlaka husika kufika na kuchukua hatua za haraka,"

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa Kibululu, Goba ni maeneo kupita Stanza, shule ya Precious kama unatokea Makongo.

# JPM kuhudhuria kuapishwa Ramaphosa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amewasili jijini Pretoria, Afrika Kusini, ambapo leo atahudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais Mteule wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa.

Rais Magufuli ambaye ameongozana na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Philip Mangula, aliwasili jana katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Oliver Tambo jijini Johannesburg kisha kuelekea Pretoria.

Rais Mteule Cyril Ramaphosa ataapishwa kuwa Rais wa 5 wa Afrika Kusini katika sherehe zitakazofanyika katika uwanja wa Loftus Versfeld jijini Pretoria.

# Mbunge matatani Stiegler's Gorge

INATOKA UK. 2

waliomba kuutekeleza.

"Na ndiyo maana tumeingia mkataba nao kwa kiasi cha Sh. trilioni sita ambazo wakandarasi na timu ya wataalamu ya serikali iliyoundwa kwa pamoja na kwa majadiliano wamekubaliana.

"Sasa, Ruge anaposema kwamba mradi utagharimu Sh. trilioni 21 na kwamba serikali imeingia mkataba na benki kugharamia mradi huo.

"Napenda nimwambie serikali kwa vyanzo vyake vya ndani na imeshatoa asilimia 15 kiasi cha Sh. bilioni 685. Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, anaposema serikali imetumia benki ambazo hazipo, asilipotoshe Bunge," Mgalu alisema.

Naibu waziri huyo alisema serikali itagharamia mradi huo kwa pesa zake za ndani na imeshalipa asilimia 15 na kazi inaendelea.

Kutokana na taarifa hiyo ya Mgalu, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa anaongoza kikao cha Bunge, alimtaka Ruge kuthibitisha kama taarifa alizoziwasilisha bungeni zina kweli na ana ushahidi au afute maneno hayo.

Alipopewa nafasi ya kuthibitisha ama kufuta kauli yake, Ruge alichokisema bungeni kinatokana na ripoti ya utafiti inayoonyesha changamoto hiyo.

"Kwa hiyo, katika yale maneno mawili, wewe unasema unao ushahidi?" Naibu Spika alihoji huku Ruge akijibu kuwa ana ushahidi wa suala hilo.

"Waheshimiwa wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu, mchango wa Mheshimiwa Catherine, nimelazimika kuuliza kwa mara ya pili kama anao ushahidi kwa sababu ameanza kwa kusema yeye ni mawazo yake.

"Lakini kwa kuwa amethibitisha kwamba yeye anao ushahidi, kwa hivyo, mimi nitamruhusu aendelee kuchangia, ataleta ushahidi wake ambao kama taratibu zetu zilivyo ili kumbukumbu zetu zikae sawasawa, utapelekwa kwenye kamati ambayo itatusaidia kuangalia uhalisia wa hiyo taarifa," Dk. Tulia aliagiza.

Kiongozi huyo wa Bunge alimtaka Ruge kupeleka ushahidi wake kwa kamati Jumatano ijayo.

**JIWE LA MSINGI JULAI**

Akichangia mjadala huo jana mchana, Naibu Waziri wa Nishati (Mgalu), alisema ifikapo Julai mwaka huu, jiwe la msingi litawekwa kuashiria kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa mradi Stiegler's Gorge.

"Itakuwa ni kupoteza muda kujadili kwa misingi ya kwamba turudi nyuma, haturudi nyuma, nataka niliseme wazi kabisa hili," Mgalu alisema.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa mradi huo unafanyika kwa kuzingatia utafiti uliofanywa na wataalamu mbalimbali, akieleza kuwa hakuna utafiti ambao umebainisha kuwa mradi huo hauna faida.

"Kwa sasa, tunapotekeleza mradi huu, imeshafanyika tathimini, hivyo sisi tumeangalia faida na hasara zake hususani kumpunguzia Mtanzania gharama kubwa za matumizi ya umeme.

"Tumetathimini vyanzo mbalimbali na kwa kuwa tunatekeleza mpango kabambe wa umeme ambao umeainisha kila chanzo kinatakiwa kizalishe megawati ngapi ili kufanya upatikanaji wa umeme uwe kwa urahisi," alisema.

Alibainisha kuwa umeme unaotokana na chanzo cha maji unagharimu Sh. 36 kwa unit, umeme unaozalishwa kwa gesi Sh. 147 na unaozalishwa kwa mafuta Sh. 526.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, pia aliuzungumzia mradi huo bungeni jana akieleza kuwa dhamira ya Rais John Magufuli kutekeleza mradi huo ni njema ikizingatiwa nchi inaelekea kwenye uchumi wa viwanda.

"Tupo tayari na tumeanza kutenda, amesema mbunge huyu (Ruge) kwamba serikali haina uwezo, naomba nimwambie kwamba tumejipanga, tumejiandaa na tuko tayari kutekeleza mradi huu na utakamilika kwa wakati na Watanzania watafaidi matunda ya serikali yao," alisema.

Aliwataka Watanzania wasikubali kutumika kwa kuwa ni taifa huru na mradi huo utatekelezwa kwa kuwa tayari Sh. bilioni 688.6 zimepelekwa kama fedha ya kuanza utekelezaji. "Pesa yake ipo, wala hatuhitaji kwenda kukopa au kuomba, ipo kwa ajili ya mradi wa umeme Mto Rufiji," Dk. Kijaji alisema.

# Madiwani wataka mwongozo

INATOKA UK. 3

msaada wa kuisukuma serikali kulipa fedha hizo," alisema Chogoo.

Alisema kutokana na kokosa fedha hizo ambazo zingewawezesha kununua pembejeo, wengi wameshindwa kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu ujao. "Nionavyo tatizo la malipo ya korosho litaathiri sana uchaguzi wa serikali za mitaa tunaiomba serikali kuwalipa wakulima wetu, kwani hali zao za maisha ni mbaya na hata sisi nafasi zetu za udiwani ziko matatani, na ndiyo maana tunachukua hatua mapema," alisema.

Diwani wa Mpindimbi, Samson Bushiri, alisema kwenye kata yake wakulima zaidi ya 68 hawajalipwa ambao wengi walikopa kwenye taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya CRDB.

Alisema kutokana na kuchelewa kwa malipo hayo, wameshindwa kurejesha mikopo na kuingia wasiwasi wa ongezeko la riba, huku wakishindwa kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu ijao.

"Kwakweli kama wawakilishi wa wananchi kwenye kata zetu tunashindwa kutoa majibu sahihi kwa wakulima wetu ambao ni wananchi tunaowaongoza kuwa lini watalipwa fedha zao kila siku wamekuwa wakituuliza," alisema na kuongeza:

"Tunaomba majibu kwani hivi sasa tunaelekea katika msimu mwingine serikali haijalipa fedha msimu uliopita."

Diwani wa Lulindi, Musa Msanga, alisema kuendelea kuisubiri serikali kushughulikia malipo ya korosho kwa wakulima ambao hawajalipwa ni kuwatesa wananchi, na kwamba wakati sasa wa kuangalia muongozo wa kisheria ili wafungue madai dhidi ya serikali.

Akijibu hoja hizo, Mwanasheria wa halmashauri hiyo, Sanga alisema suala hilo lipo ngazi ya juu kwa kuwa serikali ndiyo ilinunua korosho kutoka kwa wakulima, na kwamba watalipeleka ngazi za juu ili kuona nini cha kufanya.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Jeremia Lubeleje, alisema halmashauri inapokea hoja hiyo na wataipeleka kwenye ngazi nyingine.

# Sababu makandarasi

INATOKA UK. 3

hatujawahi kuifanya ya kukagua makandarasi yote nchini kuanzia Jumatatu," alisema Nkori.

Alieleza zaidi kuwa, operesheni hiyo itafanyika kwa makandarasi 10,122 waliyosajiliwa na bodi hiyo na wataanza na 418 wa madaraja makubwa ambao watakahikikiwa kwa miezi mitatu.

Msajili huyo, alieleza baada ya kundi hilo wataanza kuhakiki makandarasi wazalendo, wakati na wadogo na wale makandarasi maalum, kazi itakayofanyika hadi Novemba.

"Tutafanya uhakiki wa makandarasi wa ndani na nje ya nchi ambao tumewasajili, wafanyakazi wetu watawatembelea maeneo yao ya kazi, watazungumza nao moja kwa moja, kukagua miradi yao lengo ni kutaka kuona fedha zote za miradi ya maendeleo zinazotolewa na Serikali hazipotei," alisema.

Kuhusu makandarasi watakaofutiwa usajili, Nkori alisema ni wale ambao walikimbia kazi bila sababu za msingi ilihali walikubali wanaweza kufanya na wale waliotumia rushwa kupata tenda.

Aliwataja wengine watakaofutiwa usajili ni wale waliotumia anuani za makandarasi wengine kufanya kazi huku Kandarasi aliyesajiliwa akiwa hayupo eneo la mradi.

"CRB ikiwa ni chombo chenye dhamana na mamlaka ya kisheria na kuratibu, kusimamia na kuendeleza Makandarasi nchini, kwa namna ya pekee tuona makandarasi watakaobainika na miongoni mwa makosa tuliyotaja watafutiwa usajili moja kwa moja," alisema Nkori.

## HABARI ARUSHA

# Bodi ya Maji Pangani yawanoa wateja

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BODI ya Maji ya Bonde la Pangani, imeanza kutoa mafunzo kwa watumiaji wa maji wa mito mikubwa ya Themi, Kikuletwa na Naura mkoani Arusha, ili kuwawezesha kuelewa rasilimali za maji na hatimaye kuwajibika kuzilinda, kuzitunza na kuzisimamia.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa bodi hiyo, Abraham Yesaya, alisema hayo jana alipokuwa akitoa mada kwenye mafunzo ya siku moja ya kuwajengea uwezo na uelewa wadau hao yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha.

Yesaya alisema kulingana na mabadiliko ya sera ya maji yaliyofanywa mara ya mwisho, wananchi wanatakiwa washirikishwe na wawe ndio wasimamizi wakuu wa rasilimali za maji na kila Kijiji kitakuwa na kamati yake.

Alisema serikali imekuja na mkakati huo wa kutoa mafunzo kwa wananchi vijijini, ili kuelewa sheria za maji , usimamizi wake na uboreshaji wa mazingira ya mito hiyo isikauke na kuchafuliwa, kutokana na matumizi mabaya.

Aidha, alisema bodi hiyo imeshatoa mafunzo kwa watumiaji wengine wa maji wa mito mikubwa ya Nduruma na Kikuletwa wilayani Arumeru, mafunzo ambayo lengo lake ni kuwajengea uwezo watumiaji wa maji kwenye mito hiyo wataunda uongozi wa kusimamia rasilimali hizo na serikali itatoa msaada wa kiutaalamu na vitendea kazi.

Yesaya alisema kupitia mafunzo hayo, wawekezaji walioko kandokando ya mito hiyo, vikiwemo viwanda, hoteli na mashamba ya maua, watashiriki kikamilifu katika utunzaji na uboreshaji wa mito na vyanzo vingine vya maji, hivyo kusitisha utiririshaji wa maji ya viwandani mitoni.

Kuhusu uchimbaji wa visima vya maji, alishauri usifanywe holela kwa kuwa madhara yake ni makubwa na kutahadharisha kuwa kukitokea tetemeko la ardhi, itakuwa hatari kwa makazi kutokana na utitiri wa visima.



Msaidizi wa Kisheria wa Wilaya ya Hanang', Paulina Longu, akizungumzia changamoto wanazokutana nazo vijijini, katika mafunzo ya kujengewa uwezo yaliyoandaliwa na mtandao wa asasi za kiraia mkoani Manyara (Macsnet), mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbunge apania kusimamia ukweli

**Na Cynthia Mwilolezi,** KITETO

MBUNGE wa Kiteto Mkoani Manyara, Emmanuel Papian, amesema ataendelea kusimamia ukweli hata kama ni mkali kama pilipili ili mradi wananchi wapatiwe huduma wanazostahili.

Papian akizungumza juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri ya Kiteto, alisema hana hofu katika kusimamia ukweli.

Alisema baadhi ya madiwani wanataka kuonekana sukari kwa kuficha ficha mambo, lakini yeye ataendelea kusimamia ukweli kwa manufaa ya wananchi wa Kiteto.

Papian alisema kuna baadhi ya makandarasi walipata zabuni ya miradi ya maji, lakini hawajaitekeleza japokuwa wengine walishapatiwa fedha zote.

"Nitaendelea kusimamia ukweli kwenye maendeleo kwani ni kwa ajili ya manufaa ya wananchi. Sitakubali kunyamaza kwa sababu nazungumzia ukweli," alisema Papian.

Alisema suala la miradi ya maji amejitahidi kusimamia kwa kuhakikisha inakamilika lakini baadhi ya makandarasi wanawarudisha nyuma na yeye atasimama kidete kwa ajili ya manufaa ya wananchi.

"Suala la mradi wa maji wa Wazamtima tutahakikisha unakamilika kwa manufaa ya wananchi, hivyo jamii isiwe na hofu kabisa juu ya kumalizika kwa changamoto hiyo," alisema Papian.

Aliwahakikishia madiwani wa halmashauri hiyo kuwa yeye hana tatizo katika kutimiza wajibu wake kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo ameitekeleza.

Hata hivyo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Hassan Benzi, alimshukuru mbunge huyo kwa kufanikisha safari ya mafunzo ya madiwani hao bungeni jijini Dodoma.

"Safari yetu ya jijini Dodoma ilikuwa nzuri. Tumeona wabunge wakiuliza maswali tumeingia jengo la Pius Msekwa tukahoji mambo mengi tukajibiwa na maofisa wa bunge," alisema Benzi.

Diwani wa Kaloleni, Christopher Parmet, alisema ziara hiyo ya bungeni Dodoma, ilikuwa na manufaa makubwa kwa madiwani hao, kwani wamejifunza mambo mengi.

"Hii ni historia kwetu kwani madiwani tumejifunza mengi na iwe changamoto kwetu kujipanga na kufanikisha safari ya wenyeviti wa vijiji na kamati ya siasa ya CCM Kata, kwenda bungeni Dodoma," alisema Parmet.

# Wadau wa utalii wa EAC waweka mikakati

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WADAU wa utalii katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wametaka kuwapo kwa usawa wa kimaslahi na haki kwa wafanyakazi wa sekta hiyo ili kuleta tija na mapato zaidi.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Hifadhi, Hoteli, Nyumbani, Huduma za Jamii na Ushauri (CHODAWU), Said Wamba, wakati akizungumza katika kongamano la wadau wa utalii, kutoka nchi za jumuiya hiyo, lililoangalia wafanyakazi walioko katika utalii wanavyoweza kunufaika na sekta hiyo.

Wamba alisema kumekuwapo na changamoto zilizofanana katika sekta ya utalii, katika nchi zote za jumuiya na wadau hao kwa pamoja watajadili namna ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi na masuala mengine.

Kongamano hilo limeandaliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi wa Hoteli na Kilimo Duniani (IUF) na ni la kwanza kufanyika kwa nchi za EAC.

Lengo hasa la kongamano hilo ni kuangalia jinsi ya kuboresha sekta ya utalii kwa nchi hizo ili kuhakikisha maslahi yanakuwa sawa kwa nchi zote na wafanyakazi wakinufaika kupitia sekta hiyo.

"Changamoto kubwa iliyopo kwa wafanyakazi katika sekta hii, ni wengi wao kutokuwa na ujuzi wa kazi zao na kusababisha kulipwa mishahara duni, hivyo ni wajibu wa wadau katika sekta kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa mafunzo ya kuwajengea mazingira bora na hatimaye kulipwa mishahara bora," alisema Wamba.

Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Kanda ya Afrika Mashariki, Wellington Chibebe, alisema lengo la mkutano huo ni kuhakikisha waajiri na wafanyakazi wote wanapata haki sawa, katika nchi hizo, ili wote kwa pamoja kuwa na sauti moja ya kuboresha sekta ya utalii.

Naye mwakilishi kutoka nchini Kenya, Jacquline Wamai, alisema changamoto zilizopo katika sekta ya utalii kwa nchi za EAC zinafanana, hivyo alitaka kuwapo kwa sera moja itakayotumika kwa nchi hizo, huku akitaka wafanyakazi wote kulipwa haki sawa bila kujali anatokea nchi gani.

Alisema kumekuwapo na ubaguzi kwa baadhi ya nchi kulipa wafanyakazi mishahara tofauti kulingana na nchi waanazotoka, huku wageni wakilipwa mishahara mikubwa wazawa kidogo, hivyo alitaka mfumo huo kubadilishwa na wafanyakazi wote kulipwa mshahara sawa.

# Serikali yasaidia wanafunzi waliopoteza vifaa ajali moto

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HATIMAYE serikali imepeleka misaada ya awali ya kibinadamu pamoja na vifaa vingine vya kielimu kwa wanafunzi 224 wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira, ambao wamepoteza vifaa vyote katika ajali ya moto iliyotokea juzi asubuhi eneo la Marangu, Wilaya ya Moshi.

Moto huo ambao chanzo chake hakijajulikana, umeteketeza mabweni mawili ya ghorofa ya shule hiyo kongwe, lakini hadi sasa chimbuko la moto huo linaacha maswali mengi yasiyojibika Jana, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Michael Kilawila, akiwa ameongozana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, Beatrice Mwinuka na Ofisa Elimu Sekondari, Juma Tukosa, walikwenda kugawa misaada hiyo ya kibinadamu ili kuwasitiri wanafunzi hao ambao wamepoteza kila kitu.

"Ni majonzi kwa wanafunzi hawa ambao hawana hata nguo moja ya kubadilisha zaidi ya sare waliyokuwa wamevaa wakiwa darasani, wala vifaa mbalimbali ambavyo walikuwa wakivitumia kabla ya ajali ya moto, Halmashauri ya Moshi ambayo shule hii iko chini yake kiusimamizi tumeona tulete misaada ya awali kwa ajili ya kuwasitiri wasichana hawa.Tunafungua milango kwa wadau wengine kuwasaidia kwa hali na mali,"alieleza Kilawila

Mpaka sasa kuna utata wa namna moto huo ulivyojitokeza na jinsi mabweni hayo mawili ya Muungano na Japan yasiyotegemeana kwa umeme, kuungua kwa wakati mmoja. Ajali hiyo ya moto ilitokea Mei 23, 2019, majira ya saa 2:00 asubuhi.

Vifaa vilivyokabidhiwa kwa Mkuu wa Shule hiyo, Elizabeth Abdallah ni pamoja na mablanketi 103, mashuka 206, taulo 103, miswaki katoni 9, dawa ya meno katoni 9 na mafuta ya kujipaka ya vasseline katoni 9.

Nyingine ni malapa katoni 9, soksi katoni 9, daftari katoni 43 na sabuni katoni 5 ambavyo vyote vina thamani ya Sh.7, 960,500.

Kufuatia tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameeleza kuwa amepokea kwa masikitiko ajali hiyo ya moto katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira, huku akidokeza kuwa tayari ameruhusu uchunguzi kuhusu ajali hiyo kuanza kufanyika.

Sekondari ya Wasichana ya Ashira, imo katika kundi la shule kongwe za kitaifa za wasichana zilizowika miaka ya nyuma kwa kutoa wanafunzi wenye vipaji maalum, zikiwamo pia Sekondari ya Wasichana ya Weruweru, Kilakala, Msalato, Machame, Sekondari ya Wasichana Tabora na Nganza ya Mwanza.



Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Hai, SSP Lwelwe Mpina, akishiriki kupakua mifuko 200 ya saruji, iliyotolewa msaada kwa ajili ya upanuzi wa Kituo Kikuu cha Polisi cha wilaya hiyo, (Bomang'ombe), juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# DC ajibebesha jukumu la ujenzi jengo la polisi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amejitwisha jukumu la kusimamia ujenzi wa jengo jipya la upanuzi wa Kituo Kikuu cha Polisi Bomang'ombe, akiahidi ndani ya siku 90 askari watafanya kazi zao katika mazingira yanayoridhisha.

Ole Sabaya, pia ameahidi baada ya kukamilika kwa upanuzi huo, kamati ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itajenga makazi mapya ya askari wa wilaya hiyo.

Alikuwa akizungumza jana na askari wa jeshi hilo pamoja na wananchi, wakati zoezi la kukabidhi mifuko 200 ya saruji na tani moja ya nondo kwa ajili ya upanuzi wa kituo hicho. "Leo tumeanza hili, niliwaahidi na mmeona limetekelezwa na nitahakikisha jengo linakwisha.Niwaambie tu kwa sababu tumeleta mifuko hii, sitegemei kabisa mje mniambie kuna hata mfuko mmoja umepotea, nitawashughulikia. OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) nitawashughulikia.

"Hii ni sehemu ambayo kuna uadilifu, tuwaonyeshe wananchi tunavyoishi maisha ya uadilifu kwa mfano.Ndani ya miezi mitatu nitahakikisha hilo jengo linakwisha.Tutahakikisha Polisi wetu wanawahudumia wananchi katika mazingira ya kuridhisha na bila bugudha." Aidha, Ole Sabaya wakati anazungumza na askari pamoja na wananchi waliofika kushuhudia makabidhiano hayo, alisema uamuzi wa kutoa vifaa hivyo ni katika kutekeleza maelekezo ya Rais John Magufuli ya kuwasogezea wananchi huduma.

Alisisitiza: "Tumeleta kwa makusudi kwa ajili ya kufanya kazi kupanua eneo hili la Kituo cha Polisi Bomang'ombe. Kumekuwa na uhitaji huo na hiyo itawarahisishia wananchi wetu kuja kupata huduma kwa haraka na kirahisi."

Kutokana na uhitaji huo, Ole Sabaya alisema kamati ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamepambana kwa hali na mali kufanikisha upatikanaji huo wa vifaa vya ujenzi. Baada ya kupokea vifaa hivyo, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Hai, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP), Lwelwe Mpina, ameahidi saruji na nondo zilizotolewa na Mkuu huyo wa wilaya akishirikiana na kamati yake ya ulinzi na usalama na wadau wa maendeleo havitapotea na vitafanya kazi iliyokusudiwa, kwa kuwa vipo katika mikono salama.

# Wafugaji wakaidi watangaziwa kiama

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

JAMII ya wafugaji wanaoishi katika Kijiji cha Tindigani, wilayani Hai ambao wanaachia kwa makusudi wanyama wanaowafuga kuzurura ovyo katika makazi ya watu, kuharibu mazao na mashamba, siku zao zinahesabika.

Tangazo la kusitisha utaratibu huo na kuanza kuchukuliwa kwa hatua stahiki, ikiwamo kutozwa faini ya Sh. 25,000 kwa kila mfugo mmoja, limetolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya watumia maji na utunzaji mazingira wa Wilaya za Hai na Siha (Umasakwa) Goodchance Moshi.

Moshi alitoa onyo hilo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Tindigani, baada ya zoezi la kupanda miti 800 kukamilika katika Shule ya Msingi Semindu iliyopo Kitogoji cha Ukambani.

"Tumeanzisha kampeni ya kukamata mifugo inayozurura na kugeuza vyanzo vya maji kuwa eneo la malisho ya mifugo, kuingizwa kwa makusudi katika makazi ya watu na mashamba ya wakulima yenye mazao na kuharibu miti inayopandwa. Udhibiti huu unalenga kulinda na kutunza mazingira," alieleza

Moshi alisema faini hiyo hailengi kumkomoa mfugaji, bali kulinda na kuhifadhi mzingira kutokana na mifugo kuharibu miti iliyopandwa.

Akitetea uamuzi huo, Mwenyekiti huyo ameeleza kuwa haiwezekani serikali na wadau mbalimbali wa mazingira, waweke jitihada kubwa katika kupanda miti, halafu mifugo ije kuharibu kazi hiyo, ni lazima sheria ichukue mkondo wake.

Jackson Mollel ambaye ni Mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, alisema mwaka jana walipanda miti zaidi ya 250 kuzunguka shule hiyo, lakini yote ililiwa na mifugo.

Kwa mujibu wa Mollel, "Zipo sheria zinazokataza mifugo kuzurura ovyo pamoja na wamiliki kutozwa faini au mifugo kupigwa mnada, sasa hatua zitachukuliwa kwa wale wote watakaoachia mifugo kuharibu mazingira yetu."





Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai (kushoto), akisalimiana na Afisa Mkuu wa Kitengo cha Digitali, Mifumo na Bidhaa kutoka Benki ya NMB, Pete Novert, walipokutana katika Shule ya Sekondari Mnyakongo, wilayani Kongwa jana. Katikati ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Margaret Ikongo na Meneja wa Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi.
**PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Mbunge ashauri ukubwa wa nyavu upitiwe upya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeshauriwa katika mapitio ya Sheria ya Uvuvi izingatie suala la ukubwa wa nyavu za kuvulia samaki kwa kuwa limekuwa kikwazo kwa wavuvi.

Akichangia bajeti ya Wizara hiyo ya mwaka 2019/20 juzi, Mbunge wa Mafia (CCM), Mbaraka Dau, alipongeza mchakato wa serikali wa kufanyia mapitio ya sheria hiyo na kwamba kulikuwa na mgongano wa sheria hiyo na Sheria ya Hifadhi ya Bahari.

"Kuna mambo matatu ambayo unatakiwa kuzingatia kwenye mapitio ya sheria ya uvuvi, kwanza suala la ukubwa wa nyavu za kuvulia samaki, ulipokuja Waziri kule uliposema samaki watavuliwa kwa nyavu ya Inch tatu kila mtu aliguna kwa kuwa sisi kwetu kuna samaki wengine kwa asili ya maumbile yao hawakui kwa ukubwa huo," alisema.

Alieleza baadhi ya samaki wanakua kwa Inchi 1.5 ambao hata wakiachwa miaka 50 baharini hawataweza kukua kufikia Inch tatu.

"Na sisi tumeweka maoni yetu unaposema Inchi tatu kuna baadhi ya samaki hawatavuliwa maisha kwasababu tundu la ukubwa huo watapita tu," alisema.

Aidha alishukuru serikali kwa kubadili nyavu ya kuvulia dagaa kutoka milimita 10 hadi nane.

"Taarifa hizi ziende hadi chini kwa kuwa bado kuna maafisa wanasumbua kule watu licha ya utaratibu kubadilishwa,"alisema.

Pamoja na hayo, Mbunge huyo alishauri kuwe na bandari ya uvuvi kwa kuwa ni namna pekee ya kuongeza mapato ya serikali.

"Kanuni ya 0.4 kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu imewakimbiza wavuvi wakubwa wote hawaji sasa hivi, meli haziji kuvua kwenye bahari kuu," alisema.

Kadhalika, alisema zimetengwa Sh. milioni 153 kwa mwaka huo kwa ajili ya mgawo wa maduhuli katika vijiji ambavyo vipo katika hifadhi ya bahari visiwa vya mafia.

"Hizi Sh. milioni 153 zimeandikwa zinaenda vijiji 17, tumesomewa taarifa kule Jibondo kuwa vijiji vilivyopo kwenye hifadhi hiyo ni 12 tu na vitongoji vitano, hii takwimu imenistua sana maana moja ya kilio cha watu wa Mafia ni kwamba hifadhi ya bahari imekuwa ikiongeza mipaka kila wakati,"alisema.

Alisema awali vilianza vijiji 3, mara 7 mara 12 na sasa 17.

Dau pia alisema katika bajeti hiyo kuna Sh.Milioni 43 zitaendelea kutolewa mkopo kwa wanavijiji ambao wamo ndani ya hifadhi ya bahari.

"Naomba nitoe tahadhari namna ya mikopo hii itakavyotolewa, kuwapo na utaratibu mzuri maana huko nyuma mikopo ilitolewa nje ya utaratibu, fedha hazikwenda kwa walengwa," alisema.

# Ndugai ataka wananchi wapewe elimu ya fedha

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameiomba Benki ya Nmb kutoa elimu ya utunzaji fedha kwa wananchi ili wajue mamna bora ya kuhifadhi fedha zao za mikopo.

Ndugai aliyasema hayo juzi wakati uongozi wa benki hiyo waalipotembelea katika shule za Mnyakongo na Chiwe wilayani Kongwa, na kutoa msaada wa madawati 63 na meza pamoja na mabati 250.

Ndugai alisema NMB wana kila sababu ya kutoa elimu ya utunzaji fedha kwa wananchi kama wanavyofanya kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Alisema watu wengi wanakopa fedha lakini hawajui wafanyie nini baada ya kuzichukua.

Alisema watu wanaochukua mikopo wengi wao hakuna cha maana walichofanyie badala yake wanaishia kuwa na maisha mabovu.

Alisema kutokana na hilo kuna kila sababu ya elimu hiyo kutolewa kwa wananchi ili wakope wakijua wanakwenda kuzifanyia nini hizo fedha.

Alifafanua kuwa ameshakutana na kesi hizo nyingi kwa ndugu jamaa na marafiki ambao wamekopa bila ya kupata mafanikio yoyote.

Alisema hali hiyo inawaumiza sana wananchi na kusababisha kurudi nyuma badala ya kwenda mbele katika maisha kupitia fedha za mikopo.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema NMB imetenga maeneo manne kwa ajili ya kusaidia jamii.

Alisema maeneo hayo ni Elimu, Afya, Kilimo na utunzaji fedha kwa vijana hadi watu wa rika la juu kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Alisema hadi Sh. milioni 400 zimeshatolewa kwa ajili ya misaada katika shule na hospitali ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema NMB iko pamoja na serikali kuhakikisha wanafikia malengo waliojiwekea.

Naye Mkuu wa Shule ya Mnyakonga, Mpokeeni Sanga, alisema wana upungufu wa madawati 70 na wanaishukuru NMB, kwa kuwapatia msaada huo.

# Mimba za utotoni bado changamoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI ya Maendeleo ya vijana mkoa wa Dodoma (DOYODO), imesema kuwa takwimu za utafiti wa mambo ya afya (TDHS) ya mwaka 2016/2017 zinaonyesha tatizo la mimba za utotoni kitaifa ni asilimia 39, huku Mkoa wa Dodoma ukishika nafasi ya tatu.

Aidha Mkoa wa Dodoma umekuwa wa tatu kwa asilimia tatu, huku wilaya ya Chamwino ikiogoza kwa kuwa na wasichana 24 waliopata mimba.

Meneja wa mradi wa taasisi hiyo ya vijana, Charles Ruben, alisema hayo wakati alipokuwa akitoa taarifa kwenye uzinduzi wa mradi wa magauni manne iliyofanyika jijini hapa.

Alisema shule zingine ambazo zenye watoto wa kike waliopata mimba za utotoni ni pamoja na idadi yake kwenye mabano Wilaya ya Mpwapwa (13) Dodoma mjini (12) Kongwa (10) huku wilaya ya Kondoa na Kondoa mjini ilikwa na sifuli, na kufanya jumla ya wasichana wote kwa upande wa shule za msingi Mkoa wa Dodoma waliopata kuwa 67.

Aidha alisema kwa mujibu wa takwimu hizo kwa Halmashauri ya jiji la Dodoma kwa mwaka 2018 wasichana wa shule za sekondari walikuwa 45 na kwa mwaka huu toka Januari hadi machi 2019 kuna mimba 35.

Hata hivyo, alisema pamoja na matokeo hayo, taasisi imekuwa ikiendesha miradi mbalimbali kama vile ya ufyatuaji wa matofali na magauni manne ambayo imeleta muamko chanya wa kimaendeleo kwa vijana wa Dodoma toka kuanzishwa kwake mwaka 2015 hadi 2019,huku ikifanya kampeni mashuleni kwa kutoa elimu ya utambuzi juu ya madhara ya mimba za utotoni.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa mradi huo wa maendeleo ya vijana Mkoa wa Dodoma, Rajabu Selemani, alisema changamoto iliyopo kuhusiana na kampeni za kupambana na tatizo la mimba za utotoni lipo kwa watendaji wa mitaa na kata.

Selemani alisema viongozi hao wamekuwa hawatoi ushirikiano wa kina kwenye maeneo yao na mradi huo wa magauni manne ambao umelenga kutokomeza mimba za utotoni katika mkoa wa Dodoma.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, aliwataka watendaji hao kutokuwa kikwanzo cha kampeni hiyo kutofikia malengo yake ikinzingatiwa kuwa ni sehemu ya msaada wa serikali katika kupambana na suala hilo la mimba za utotoni.

"Falsafa ya magauni manne inalenga kutokomeza mimba za utotoni Mkoa wa Dodoma ikimaanisha gauni la kwanza ni sare ya shule, la pili joho la mahafali, tatu ni la harusi na mwisho ni martenity mama wajawazito," alisema na kuendelea:

"Hivyo falsafa hii inalenga kutoa elimu ya madhara ya mimba za utotoni mkoani hapa ikiwa na maana kuwa mwanafunzi au kijana anatakiwa kuvaa magauni manne kwa mtiririko sahihi ili wafikie ndoto zao."

# Wachachamaa ucheleweshaji kesi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuharakisha upelelezi wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kufikishwa mahakamani watuhumiwa.

Akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha wa 2019/20, Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub, alisema kesi nyingi zimekuwa zikichelewa kufikishwa mahakamani kutokana na kuchelewa kukamilika kwa ushahidi.

Alisema kesi nyingi ziko katika ofisi za DPP huku zikisubiri uchunguzi wa kina kukamilika kabla ya kupelekwa mahakamani.

Mwakilishi huyo alisema kitendo cha kuchelewa na kuchukua muda mrefu kabla ya kesi hizo kufikishwa mahakamani kimeibua malalamiko mengi na kuitia doa ofisi ya DPP.

Naye Mwakilishi wa Mpendae, Mohamed Said Dimwa, alitaka kujua kwa nini sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi mwaka jana imekuwa ikitoa dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya ubakaji.

Dimwa alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, dhamana ya wabakaji itakuwa ikitolewa na Jaji Mkuu kwa mazingira atakayoyaona yanafaa lakini hivi sasa wananchi wanalalamika dhamana kwa watu hao zimekuwa zikitolewa holela.

"Mheshimiwa Spika tufahamishwe kwa nini sheria tuliyoipitisha kwa wabakaji kunyimwa dhamana imekuwa haitekelezwi kwa mujibu wa sheria," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Viti Maalumu, Panya Ali Abdalla, alihoji matukio ya mwenendo wa kesi za jinai za watuhumiwa wa ubakaji ambao wamekuwa wakipewa dhamana mbele ya mahakama.

Alisema lengo la sheria hiyo ni kudhibiti vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambavyo kwa mujibu wa takwimu za mwaka mmoja vimekuwa vikiongezeka kwa kiasi kikubwa.

"Namwomba Waziri aje atuambie kwa nini watuhumiwa wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji wamekuwa wakipewa dhamana na mahakama," alisema.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na uongozi wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika mkutano wa Utekelezaji wa Mpango Kazi, kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# AG aweka wazi sheria ya mavazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Said Hassan Said, amesema sheria ya kudhibiti mavazi yanayofaa kutumiwa na Wazanzibari kwa ajili ya kulinda mila na utamaduni wao ipo na inahitaji kufanyiwa kazi. Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliochangia katika hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria. Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba hiyo, walitaka kujua kwa nini serikali haitayarishi sheria itakayodhibiti mavazi ya utamaduni wa kitaifa.

Mwanasheria Mkuu huyo alisema Sheria ya Mavazi ya Zanzibar ipo tangu mwaka 1973 ambayo ni sheria namba moja ya mwaka 1973 na inajulikana kama Sheria ya Kulinda Utamaduni wa Kitaifa. "Nimeiona Sheria ya Mavazi ya Zanzibar na nimeileta na kumkabidhi Mwakilishi Panya wa nafasi za wanawake kuisoma na kuipitia. Zanzibar inaongoza kuwa na sheria nyingi ingawa tatizo ni utekelezaji wake na usimamizi," alisema.

Alisema sheria hiyo imeweka vizuri utaratibu na aina gani ya mavazi ambayo wananchi wanalazimika kuyatumia ikiwamo wanawake na wanaume.

Pia alisema katika sheria hiyo hakuna mwanya na nafasi ya kuwapo kwa mavazi yanayokwenda kinyume cha maadili na heshima ya binadamu.

"Mheshimiwa Spika, sheria kitu kimoja na utekelezaji wake jambo lingine. Wazazi ndio wanaowanunulia nguo za ajabu watoto wao na kuwashajihisha kuzitumia," alisema.

# SMZ kufungia magari mabovu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda, imesema ina mpango wa kuyafungia magari ya abiria aina ya Convoy yanayotoka nchini Uingereza kuingia Zanzibar ili kuepusha Zanzibar kuwa dampo la magari chakavu yaliyotumika kwa muda mrefu.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema mpango huo unafanyiwa kazi na utakapokamilika utapelekwa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

Balozi amina aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mtambile, Mussa Foum Mussa, ambae alitaka kujua wizara inatumia mbinu gani kudhibiti vitu chakavu ikiwemo magari yanayoingizwa zanzibar na baadhi ya wafanyabiashara.

Alisema wizara itahakikisha jambo hilo linashughulikiwa ili Zanzibar isiwe chaka la kuletwa magari mabovu.

Alisema kupitia masuala ya kodi kuna viwango vilivyowekwa kwa magari makuu kuu yanaingizwa Zanzibar, hivyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeweka kodi kubwa ili wafanyabiashara wasiyalete magari hayo na kuhakikisha yale yanayoingia nchini yanakuwa imara.

Naye Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Ameir Hafidh, alisema hatua hiyo itaondosha dhana kuwa baadhi ya wafanyabiashara kuifanya Zanzibar kuwa dampo la vifaa chakavu.

Alisema serikali inayafanyia ukaguzi magari yote kabla ya kufika nchini na mengine kukaguliwa wakati yakiingia Zanzibar.

Alisema, yako malalamiko mengi yaliyopokewa katika ofisi yao yanatokana na magari hayo na wizara imeanza kuyafanyia utafiti kupitia timu ya wataalamu wa Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS).

Naibu waziri huyo aliitoa wito kwa wafayabiashara ambao tayari wameshaagizia magari hayo wasiyalete kwa kuwa hatua zitachukuliwa na kuwasababishia kuingia hasara.

Alisema serikali imeanzisha tasisi mbalimbali za viwango kwa ajili ya kuvikagua na kuhakikisha vifaa vyote vinavyoingia vinakuwa na viwango na bidhaa ziko salama kwa matumizi ya binadamu.



Soma UK. 15

KONKI

JUMAMOSI MEI 25, 2019

Nipashe

BT

BURUDANI TELE



# KONKI KONKI KONKI MASTER KWA HILI NAKUPA TANO

UK.16

BASI SAWA





## Beka Flavour atoa siri bifu la Aslay, Mbosso

NYOTA wa muziki wa Bongofleva, Beka Flavour amesema kuwa ameshtushwa na kushangazwa na mtafaruku uliopo kati ya wasanii wenzake, Mbosso na Aslay unaoendelea mitandaoni.
Akizungumza na kituo kimoja cha televisheni, Beka amesema kuwa alimuona Mbosso kwenye moja ya mahojiano akimtuhumu Aslay kuwa amemu-unfollow na hana sapoti ya kutosha kwake, ingawaje yeye amekuwa akimuoneshea upendo kwa kusapoti kazi zake.
Hivyo na yeye (Mboso) ameamua amuondoe kwenye ukurasa wake wa kijamii wa Instagram.
Beka Flavour amesema yeye ni kaka yao na kipindi cha nyuma alikuwa anawashauri lakini kwa sasa hawezi kufanya hivyo kwa sababu kila mtu yupo na uongozi wake.
Wasanii hao kwa pamoja walikuwa wanaunda kundi la Yamoto band ambalo kwa sasa halipo tena.



## Ferooz: Saa hizi ukitoa pini kali unatoboa

MKONGWE wa bongofleva Ferooz ameweka wazi kuhusu maisha yake na kuwazungumzia wasanii wenzake ambao wanajipendekeza kwa wale wenye mafanikio makubwa hasa fedha.
Akizungumza na safu hii, Ferooz amesema maisha yamebadilika kwa kiasi kikubwa kwenye gemu, kwani hivi waliotumia nafasi vizuri wanaingiza mkwanja mrefu.
"Kifupi mimi maisha yangu kipindi kile sio sawa na sasa, yaani napigana kurudi tena kwenye ramani, lakini kiukweli kwa sasa ukiwa makini unatoboa kirahisi zaidi," alisema Ferooz.
Ferouz ambaye ni mmoja wa wasanii waliouweka kwenye ramani muziki huo kwa sasa amerudi upya na singo yake mpya aliyoipa jina la Excellent aliyomshirikisha mkali wa hip hop, G Nako na pini hilo limepikwa kwa produza Mocco Genius.



# Niki 'auza' sura ya mtoto wake mtandaoni

MWANAFAMILIA kutoka kundi la Hip hop la Weusi kutoka Arusha, Niki wa Pili, kwa mara ya kwanza ameonyesha sura mtoto wake wa kike ambaye amezaliwa majuzi.
Niki alionyesha sura ya mtoto wake huyo ambaye ni wa kike kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.
Katika picha hiyo Niki aliandika: "Habari! Dunia semeni Hi kwa mtoto wangu zuri."
Aidha alitaja jina la mtoto wake huyo wa kike kuwa anaitwa Zuri.
Niki ambaye tayari ameshamchumbia mpenzi wake Joan miezi kadhaa iliyopita walibahatika kumpata mtoto huyo Aprili 23 mwaka huu siku ya Alhamisi.
Niki sasa anakua miongoni mwa mastaa ambao wamebarikiwa kupata mtoto kwa mwaka huu wa 2019.

## INSTA-TWITTER





**Asante** Mungu, nimerudi home salama, hapana chezea dengu yule mbu ni bishoo, lakini anakukaza kweli. Niwape pole ndugu zangu mliostushwa na habari za mimi kutangulia mbele ya haki. Mimi mzima bado Mungu hajanipangia, siku ikifika hata aliyenipostim leo hatokuwa na bando kwa laana ya kusingizia watu- **Babu Tale.**



**Babu** Tale, sasa na lile group la mchango wa kusafirisha mwili nilivunje au tubadili jina?-**Madee Ali.**



## Nandy kumbe alikuwa na nyodo kinoma

DOGO anayechipukia kwenye bongofleva, Marioo ameibuka na kusema kwamba, msanii wa kike, Nandy aliwahi kumuwekea pozi na 'kumchomesha mahindi'.

Marioo ambaye ameandika masongi makali kama 'nabembea' ya Ditto na 'wasikudanganye' ya Nandy na sasa yeye mwenyewe yuko kwenye gemu.

Marioo amesema kati ya wansanii ambao hawakumuamini kabisa kwenye kuwaandikia nyimbo ni Nandy ambae anasema alimuwekea pozi siku ya kwanza.

"Wakati ule jina langu lilikuwa dogo, hakuna aliyekuwa anamjua Marioo na wakati natakiwa kumuandia wimbo Nandy aliniweka sana, nikamsubiri mno na ilionyesha kama kanidharau," amesema Marioo.

Hata hivyo, Marioo anasema kwa sasa kila kitu kimebadilika na mambo yanakwenda sawa, kwani jina lake ni kubwa.




@burudanitele

>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...

# Dudubaya aja na dongo la aina yake kwa wenzake



MKALI wa kitambo wa muziki wa bongofleva, Dudubaya, ameonyesha mjengo anaoishi huku akiwatupia dongo baadhi ya wasanii wenzake kwa kusema kuwa wanaishi kwenye chumba kimoja.

Dudubaya ambaye jina lake halisi ni Godfrey Tumaini alisema kwamba yeye anaishi kwenye nyumba yenye hadhi, lakini wasanii wengine tena maarufu wanaishi kwenye chumba kimoja.

"Mimi nimeamua kuonyesha mjengo ninaoishi kwa sababu nataka kuwaonyesha watu kwamba sina njaa kihivyo, hivyo naishi sehemu ya maana kabisa," alisema Dudubaya kwa jeuri.

Aliongeza kusema kuwa wasanii wengi tena wenye majina makubwa wanaishi kwenye chumba kimoja, huku yeye anaishi kwenye nyumba kubwa na yenye hadhi.

## BODA 2 BODA



# Konki amkosha Jokate

PIERE Liquid maarufu kama Konki ambaye ni mchekeshaji, ametimiza ahadi yake kwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo aliyoitoa Machi mwaka huu katika harambee ya tokomeza zero.

Katika kampeni hiyo ambayo Piere aliahidi kiasi cha Sh. laki moja, lakini amepeleka madawati wanayozidi thamani ya kiasi alichoahidi kwa kupeleka madawati ishirini.

Baada ya kupokea madawati hayo DC Jokate ameandika kuwa; "Leo nimepokea madawati 20 yenye viwango vya juu kutoka kwa Piere Liquid." Machi 31, 2019 Piere aliahidiwa na Jokate kupewa tenda ya kutengeneza madawati katika shule inayotarajiwa kujengwa wilayani humo.

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Fikiria** unavyomuogopa baba yako, halafu kuna kabinti tu tena kadogo, kanamwandikia baba yako. Acha hizo, hebu nitumie hiyo pesa haraka-**Roma Mkatoliki**.



**Hapa** ndio mimi napataga wasiwasi kuhusu, ubosi wako jamani! Yaani bado roho inakuuma kuhusu Hamisa?- **Maimatha Jesse.**



**Nilikuwa** nasafisha nyumba na mwenzangu. Mara kasinzia kazi zote kaniachia mimi- **Faiza Ally.**

# Kuumbe!

## KONKI KONKI KONKI MASTER KWA HILI NAKUPA TANO



**Na Adam Fungamwango**

DUDU Baya ni msanii mkongwe nchini asiyetabirika na mwenye tabia ya kuongea chochote kile ambacho yeye anaona kinafaa kuongelewa kwa wakati huo, bila ya kujali athari zake.

Mwishoni mwa mwaka jana hadi mwaka huu, amekuwa maarufu sana kutokana na tabia yake hiyo.

Safari hii amekuja na mpya ya kudai kuwa baadhi ya wasanii wengi wa bongo fleva na bongo movie wamekuwa wanaishi maisha ambayo si halisi machoni mwa jamii inayowazunguka, kitu kinachowatia majaribuni.

Dudu Baya ambaye kwa sasa anajulikana na Konki Konki Konki Master, amesema kuwa baadhi ya wasanii wamekuwa wakiigiza maisha na kujifanya wana aina fulani ya maisha ya juu, wakati kiuhalisia, si kweli.

'Tabia hii inasababisha mpaka baadhi ya wanafunzi huko mikoani wanaacha shule na kukimbilia mijini kuja kuigiza au kuwa wasanii wa bongo fleva ili wawe kama fulani, wakati kiukweli maisha yake si vile ambavyo anayasema yeye au yanayoripotiwa. Kusema kweli maisha ya kuigiza kwa wasanii yanaharibu jamii" anasema.

Konki anasema kuwa hakatai kama muziki haulipi, lakini ikija kwenye mgawanyo, msanii anabaki na kidogo, hivyo si rahisi sana kuwa na maisha ambayo watu wanaaminishwa.

"Sina nia mbaya nao, lakini kama mtu unapanga sema napanga, kama una nyumba umejenga nyumba ya vyumba viwili Vikindu (Mkuranga) sema, siyo unadanganya kuwa una mjengo mkubwa Mbezi Beach." alisema Konki.

Anasema kuwa athari za maisha feki ya wasanii kuonekana mazuri, wakati mwingine huja kuonekana wanapofariki dunia.

"Tumeona baadhi ya wasanii wamepofariki ndiyo tukajionea kuwa kumbe jinsi walivyokuwa wanaishi hayakuwa maisha halisi. Wengine tuliwasafirisha na kukuta kwao kuna matatizo makubwa.

"Kuna msanii mmoja mkubwa alikuwa anaendesha magari makubwa na ya kifahari, lakini kule kijijini baba yake alianguka na basikeli, watu wakawa wanamlaani msanii huyo kuwa anaendesha magari mazuri, wakati baba yake ana basikeli, kwa nini asimpe moja, kumbe yake magari si ya kwake?" anahoji.

Aliyoyasema msanii huyu mkongwe si ya kupuuzwa, kwani wanaonekana kwenye maisha ya wasanii wengi nchini.

Wamekuwa wakijifanya wanaishi maisha mazuri au ya juu, wakati si kweli na hii inasababisha hata wizara inayodili nao, isiweke sana mkazo wa kuwasaidia kuweka haki zao vizuri, ikidhani kuwa wanafanikiwa mno kutokana na kazi zao wakati si kweli.

Ukweli unabaki palepale kuwa wasanii wamekuwa wakiishi maisha ya kawaida na duni kutokana na malipo na kipato kidogo licha ya vipaji vya vikubwa walivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu.

Ilitegemewa nao wenyewe kuungana na kuwekwa ukweli kuwa hawaishi maisha mazuri na wala hawapati malipo mazuri kiasi cha kuweza kumiliki majumba makubwa kama wasanii wa Nigeria, Uganda na Afrika Kusini, ili wasaidiwe mambo yao kuwa sawa, badala yake wanakufa na tai shingoni. Nani awasaidie? Nani amfunge paka kengele? Je ni mpaka Konki Master aseme?

## WASANII BONGO WALIOPIGA 'KOLABO' NA WENZAO NJE



**Na Adam Fungamwango**

DUNIA kwa sasa imekuwa kijiji kwenye nyanja zote, iwe siasa, uchumi, kijamii na hata kwenye masuala ya muziki.

Wasanii wa sasa wana fursa ya kuungana na wenzao kutoka mataifa mbalimbali na kutoa ngoma kwa pamoja.

Mfano msanii wa Bongo, anaweza kutoa ngoma na msanii wa Kenya, Uganda au hata nje ya Afrika.

Hii ni katika kutafuta kile kinachoitwa kubadilisha ladha ya muziki, pamoja na kutafuta kuungwa mkono na mashabiki wengi, kwa sababu sasa muziki pia umeingia kwenye mitandao ya kijamii.

Hivyo, kutafuta idadi kubwa ya watu watakaofuatilia kwa kuangalia mtandaoni na hii nayo ni moja ya njia ya kujipatia kipato kwa wasanii kwenye dunia ya leo.

Wenyewe wanaita 'kolabo.' Hapa Tanzania, wasanii wengi, mbali na kupiga 'kolabo' na wasanii wenzao wa hapa hapa nchini, pia baadhi wanapiga na wasanii kutoka nje ya nchi

Hawa ni baadhi ya wasanii wa Kibongo, ambao wameshafanya 'kolabo', na wasanii kutoka nje ya nchi.


**Harmonize ft Yemi Alade-'Show Me Want You Got'**

Msanii Harmonize kwa siku za karibuni amekuwa hashikiki kwa kufanya 'kolabo' za kufa mtu na wasanii mbalimbali wa nje wa nchi, Afrika na nje ya Bara la Afrika.

Moja ya 'kolabo' yake ya hatari aliyoifanya ni dhidi ya msanii maarufu wa kike Yemi Alade wa nchini Nigeria.


Kitu ambacho Harmonize amekitoa na Alade ni 'Show Me Want You Got'. Ni kitu ambacho kimezidi kumpa heshima msanii huyo.

**Ali Kiba ft Yvonne Chakachaka-'Akili ya Mama'**



Ali Kiba, mmoja wa wasanii mwenye mashabiki wengi nchini Tanzania, ametoa ngoma nyingi kuwashirikisha wasanii mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi, lakini 'kolabo' iliyompa umaarufu mkubwa ni ile aliyofanya na 'Mama Afrika', mwimbaji wa siku nyingi Afrika, raia ya Afrika Kusini, Yvonne Chakachaka. Ngoma inaitwa 'Akili ya Mama'

**Rayvanny ft Willy Paul-'Mmmhhh'**



Rayvanny, ni msanii mwingine wa Kibongo mwenye ushawishi mkubwa kwa mashabiki nchini.

Katika moja ya 'kolabo' zake zilizompatia sifa ni ile aliyofanywa na msanii mwezake maarufu wa Kenya Willy Paul. Wenyewe walipokaa chini ngoma hiyo wakaipa jina la 'Mmmmh'


**Vanessa Mdee ft Reekado Banks-'Bambino'**



Msanii Vanessa Mdee, ni mmoja wa wasanii wachache wa kike ambao wanafanya sana 'kolabo' na wasanii wa nje ya nchi.

Ameshawahi kufanya 'kolabo' ya nguvu na msanii kutoka Nigeria, Reekado Banks na kutoa ngoma moja kali inaitwa 'Bambino'.

**Nandy ft Willy Paul-'Hallelujah'**



Nandy naye amekuwa mmoja wa wasanii wa Kibongo ambao wameingia kwenye rekodi ya kupiga 'kolabo' na wasanii wa nje, alipomtafuta Willy Paul wa Kenya na kutoa ngoma moja inayoitwa 'Halleyujah'.

# Vijimambo

1. Ndio maana wenye baiskeli hawapati ajali kama boda-boda, wanatii sheria - Kibibi, Buguruni.
2. Huyo mlugaluga ndio baiskeli yake ya kwanza nini? Ha ha haaaa! - Mama Nah, Manzese DSM.
3. Angalia jeki kama imekaa vizuri, isije ikafyatuka baiskeli ikakuua - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
4. Apewe tuzo ya usalama barabarani - Shirima, Morogoro.
5. Huyo ndio kilaza zaidi ya kilaza mwenyewe. Tangu lini baiskeli ikapigwa jeki? - Otto Mwangosi, Njombe.
6. Ama kweli ni vijimambo. Baiskeli imepigwa jeki?! - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
7. Oyaa, mbona hujavaa overoli? Oili ikimwagika itakuchafulia miparo yako - Mariam Bebeali, Migombani Zenji.
8. Mnashangaa nini? Hii sio kama basikeli zenu na shilingi mia hamsini - Masomanyika Mnambenga, Mtwara.
9. Heeee, kumbe hata baiskeli zapigwa jeki! Tobaaa! - Mwanaharusi Shemweta, Kwanjeka Tanga.
10. Huyo jamaa yenu NIPASHE kweli zimo au ndio maji kupwa maji kujaa? - Edgar Zampole, Mafinga Iringa.
11. Sio tu kadata, bali kanyongorokota. Ila baiskeli ikimuangukia atajifunza - Lina Zampole, Mafinga Iringa.
12. Ngoja nisubiri mpaka nione mwisho wake. Ataitengenezaje na atashushaje jeki - Mama Nah, Manzese DSM.
13. Hapo ni mapokezi tu Mirembe Hospital, bado kabisa hajafikishwa wodini - Maimuna Lali, Msalato Dodoma.
14. Kweli mtu chake. Haya baba ukishindwa kutengeneza ita 'breakdown' - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
15. Nahisi injini inamwaga oili. Ngoja nipige jeki nihakikishe hii oil inatoka wapi - Juma Makenika, Mwenge DSM.
16. Wewe unatuzingua wenye magari, binua baiskeli juu chini uzibe pancha uondoke zako - Munira Ali Ussi, Zenji.
17. Daaah, kweli duniani kuna mambo - 0713 998 842.
18. Hiyo inaitwa kupatwa kwa akili chafu. Hizo si akili za kawaida kabisa! - 0713 998 842.
19. Mshaambiwa, mkishangaa ya Musa mtayaona ya Firauni. Haya ndiyo ya Firauni sasa! - Kite, Sakina A Town.
20. Hivyo hivyo babake, kwani jeki iliwekwa ya nini kwenye baiskeli? - Kite, Sakina A Town.
21. Huyu kweli mzima? Mzima kabisa kabisa? Siamini - Kisinga, Magomeni Mapipa DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**

Nahisi injini inamwaga oili, ngoja nipige jeki nihakikishe hii oil inatoka wapi - Juma Makenika, Mwenge DSM.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0682 808 694**




## Mungu hakupi kilema, akakukosesha mwendo

**Na Adam Fungamwango**

BADO natafuta ni filamu iliyoongozwa na muigizaji mkongwe wa filamu, Jacob Stephen aka JB na mtunzi wa hadithi hii ni Danil Manage. Ni hadithi inayoelezea maisha ya halisi ya mapenzi jinsi yalivyo na nguvu.

Salim Ahmed aka 'Gabo' ambaye ndani ya filamu hii ametumia jina la James ndiye mhusika mkuu.Amevaa uhusika wa kijana masikini muuza maji aliyetumia matatizo yake kama changamoto na kuja kufanikiwa.

Hii ilikuwa baada ya Patricia 'Shamsa Ford' mtoto wa familia ya kitajiri ambaye alikuwa daktari kumpenda James, aliyempa ujauzito ilhali James hana mbele wala nyuma. Washiriki wengine ni Patcho Mwamba, Zuberu Mohammed, Wellu Sengo, Farida Sabu, Careen Hussein, Magdalena Roy, Mariam Adam na Hansley Andrew.

Mtunzi wa hadithi aliangalia maisha ya halisi ya mapenzi katika jamii yanayokabiliwa na migogoro, shida chuki na furaha. Patricia anazimika na penzi la muuza maji James, kitu ambacho kwa hali ya maisha ya kawaida hapa Tanzania na duniani kote hutokea kwa nadra.

James muuza maji na fundi magari mwenye maisha duni. Biashara ya maji na ufundi magari wake ulimuunganisha kimapenzi na mwanadada 'Patricia' ambaye ni daktari. Anajikuta akibeba ujauzito wa James, hali ambayo inamfanya jamaa kumuaga mwanadada huyo na kwenda kutafuta maisha ili atakapojifungua, mtoto aje kupata maisha bora kutoka kwa wazazi wake.

Shamsa mmoja ya wasanii wa filamu hapa nchini katika filamu hii ametumia jina la Patricia, baada ya kupewa ujauzito na James, watu wengi wanashangazwa akiwemo mdogo wake na rafiki zake, wakijiuliza ni kwa nini amempenda James muuza maji, wakati alikuwa nafasi wa kumpata mwanaume mwenye pesa.

Baada ya kujifungua na kukaa muda mrefu bila mawasilano na James, Patricia anapata mchumba mwingine, hali ambayo inamfanya James kushindwa kurudi nyumbani moja kwa moja akitokea katika safari ya muda mrefu ya kwenda kutafuta pesa ili waje kuishi pamoja na mtoto wao.

James anaendelea kukaa katika hoteli akitafuta jinsi ya kuoanana na Patricia,wakati huo huo anaona bora amtafute mtoto wake ili ajue Patricia anaishi na nani. Kwakuwa kabla ya kuondoka James aliacha jina la mwanaye pindi atakapozaliwa, ilimpa urahisi kumfuatilia mtoto wake katika shule mbalimbali na baadaye kufanikiwa kupata.

Anaendelea kuwa karibu na mtoto wake, mpaka pale mtoto anapokuja kumjulisha kuwa mama yake anaishi na 'Uncle' ambaye ni mchumba mpya wa Patricia na kumfanya James ajisikie vibaya sana.


Patricia anawasili katika hoteli anayoishi James, baada ya kupewa taarifa na rafiki yake kwamba yupo hotelini. Kwakuwa mlango haukufungwa Patricia anausukuma mlango na kuingia ndani.

James anajaribu kumwambia mwenzake maneno haya "Moyo wangu ulikuwa mbali lakini unaendelea kutambua, uwepo wa thamani ya mapenzi yangu kwako, moyo huu huu uliweza kugusa wa kwako wakati hauna kitu, na moyo huu huu ndio umerudi tena kwa mara nyingine kukumbusha mateso uliyopata wakati uko mbali na mimi. Moyo wangu umekubali kusamahe, kwanini wa kwako usisamehe?"

Patricia kwa hasira anarudi nyumbani na kumwambia mpenzi wake anayeishi naye wavalishane pete ili ajaribu kumsahau James. Naye James akiwa mwenye hasira anamtembelea rafiki yake ili apate ushauri. "Unajua watu wengine wanatafuta mke wa kuishi naye, lakini mimi natafuta mwanamke ambaye siwezi kuishi bila huyo mwanamke," anasema. Rafiki anamshauri James waelekee huko huko ambako Patricia anavishwa pete ili akaseme ya moyoni mbele ya kadamnasi.

Mbele ya kadamnasi ya watu, waakati ya hafla ya uvalishaji pete kati ya Patricia na mchumba wake, James anaongea maneno hata " Mapenzi yanauma asikwambie mtu, kila mtu anaelewa ,watu wote wamekuja kukuangalieni ninyi hapo sababu ya mapenzi tu na mimi kuja kote huku ni kwaajili ya mapenzi nakupenda sana mke wangu."

Maneno hayo ya uchungu yanabadilisha kila kitu na mtazamno wa kila mtu. Hatimaye James akabidhiwa mwanamke anayempenda Patricia na mtoto wake.



# JENNIFER
## AFUNGUKA MARA YA KWANZA KUTEMWA NA BRAD PITT

**LOS ANGELES, Marekani**

JENNIFER Aniston amebainisha kwamba, alikutana mara moja tu na Angelina Jolie kabla ya kuachana na Brad Pitt.

Nyota huyo wa muvi ya 'The Friends' alijulikana zaidi alipocheza kama Rachel Green kwenye muvi hiyo na mzaliwa huyo wa jijini New York City alikutana na Brad mwaka 1998.

Mahusiano yao kati ya Aniston na Brad ambaye alitamba mno kwenye filamu ya Fight Club yalitangazwa mno na vyombo vya habari.

Wawili hao waliamua kuoana mwaka 2000, baada ya miaka miwili ya mahusiano kwenye ndoa ilitofanyika kule Malibu.

Lakini walitangaza kuachana mwaka 2005, na baadae kukamilisa talaka yao huku magazeti yakimuandika Brad kuwa hakuwa muaminifu mwenye ndoa yake na Aniston. Steringi huyo wa muvi ya 'The Ocean's 11' alituhumiwa kujiingiza kwenye penzi jipya wakati akipiga picha ya muvi yake mpya ya Mr. & Mrs. Smith akicheza na Jolie, ambaye baadae alianza nae uhusiano kabla ya kuachana.

Aniston alizungumzia kuhusu talaka yake Januari 2015 wakati wa mahojiano yake na The Hollywood Reporter, alisema kwamba: "Hakuna yeyote aliyefanya jambo baya... ilikuwa tu hivyo, vitu kama hivyo hutokea."

Na sasa Jennifer ametoboa siri na kubainisha kwamba alikutana na Angelina mara moja tu kwenye maegesho ya magari wakati wa upigwaji wa picha ya muvi ya 'Friends'.

Akizungumza na jarida la Vanity Fair juzi, Jennifer ameamua kuzungumzia jambo hilo kwa mara nyingine akisema: "Nilitoka kwenye gari na nikajitambulisha mimi mwenyewe.

"Nilimuambia, 'Brad ana hamasa kubwa ya kufanya kazi na wewe. Natumaini mtapata wakati mzuri zaidi pamoja.'"

Aniston ameongeza "Kamwe kwenye maisha yangu sikusema kwamba sihitaji watoto.

"Sikufanya hivyo na bado nina matumaini siku moja nitapata!... Sitaweza kukata tamaa kamwe katika maisha haya."

Aniston pia amebainisha kwamba talaka hiyo ndiyo iliyomfanya aamue kumtafuta mama yake mzazi, ambaye alitengana nae kwa zaidi ya muongo mmoja.

Hali iliyopelekea mama yake Aniston, Nancy kuchapisha kitabu alichokipa jina la 'From Mother and Daughter to Friends'.

Aniston pia amebainisha kwamba alikuwa na msongo wa mawazo kwamba angekufa kwa sababu ya kutoweza kuzaa hadi sasa, na kusema kwamba hiyo ilikuwa sababu kubwa ya kuachana kwake na Brad ambaye amebainisha kwamba bado yupo moyoni mwake.

Amesema mahusiano yake na Brad hawezi kuyajutia kamwe na kusema kwamba kilikuwa kipindi kizuri zaidi na kilichokuwa na nyakati bora zaidi kulikowa wakati mwingine wowote.

**Jennifer Aniston, alipokuwa na Brad Pitt.**

# Kodak Black afungwa jela ya kijasusi




**LOS ANGELES, Marekani**

MWANAMITINDO maarufu nchini Marekani, Kodak Black ameingia tena kwenye mkono ya sheria akiwa anaelekea kutumbuiza kwenye tamasha la Rolling Lound usiku wa kuamkia leo kwa makosa ya silaha.

Imeripotiwa kuwa baada ya uchunguzi wa muda mrefu rapa huyo alikamatwa na vikosi vitatu, shirika la pombe, Tumbaku na silaha ATF pia walikuwepo Miami -Dade Police Northside Gang Unit, pamoja na U.S Marshals tayari amefikishwa kwenye jela ya kijajusi mjini Miami.

Matatizo ya kisheria yamezidi kumuandama rapa Kodak Black baada ya kukamatwa siku kadhaa zilizopita akiwa na silaha pamoja na dawa za kulevya kwenye gari lake.

Hata hivyo kodak amekuwa akikamatwa mara kadhaa na askari na kukutwa na silaha kinyume cha sheria huku akisitisha mara kadhaa ziara zake za muziki.



## Cardi B aahirisha tamasha kisa upasuaji

KUTOKANA na upasuaji wa kuongeza mwili alioufanya rappa Cardi B umesababisha kujitoa kutumbuiza kwenye tamasha la 92Q Spring Bling lililopangwa kufanyika ijumaa hii mjini Maryland.

Kwa mujibu wa mtandao wa TMZ rapa Cardi B amejitoa baaada ya kupata tatizo mara tu baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuongea baadhi ya sehemu za mwili wake.

Kwa mujibu wa vyanzo vya karibu vya rapa huyo vimeeleza kuwa kwa sasa yupo kwenye mchakato wa kupona baada ya kufanya pia upasuaji wa maziwa yake.

Hata hivyo, madaktari wameshauri kuwa Cardi B anahitaji mapumziko ya muda mrefu ili mwili wake urudi kama zamani kutokana na baadhi ya sehemu alizofanyiwa upasuaji kuwa hazijapona vizuri.

## Jussie Smollet yamkuta makubwa

MKALI wa tamthilia ya Empire, Jussie Smollet, anayetambulika kama Jamal katika tamthilia hiyo, amejipalia kaa la moto baada ya kutuma barua kwenye kampuni ya FOX ya ubaguzi wa rangi.

Jussie alijisalimisha mikononi mwa Polisi ili kusikiliza mashtaka yake ya kuwadanganya Polisi kuhusu kutekwa Chicago.

Kwa mujibu wa mtandao wa TMZ mwigizaji huyo ana nafasi ndogo ya kushiriki katika msimu mpya wa tamthiliya ya Empire ambayo inatajwa kuonyeshwa mwaka 2020 baada ya FOX kutangaza rasmi msimu ujao wa Empire.

Mtandao wa televisheni ya FOX umetangaza kuwa msimu wa sita ndio utakua wa mwisho wa tamthiliya hiyo ya Empire na inapanga kufanya onyesho kubwa la televisheni.





## Selena ainyooshea kidole mitandao ya kijamii

NYOTA wa filamu na muziki Selena Gomez mwenye umri wa miaka 26, amesema mitandao ya Kijamii imeharibu maisha ya vijana wengi duniani na haiwezi tena kuwa sehemu salama.

Amesema mitandao inaweza kutumika vizuri ila hata baada ya vijana kuishi katika mitandao ya kijamii bado hawajui habari muhimu.

Selena mwenye wafuasi milioni 150 alikuwa mtu maarufu zaidi kabla ya kupitwa na Cristiano Ronaldo mwenye wafuasi milioni 160.

SAFU



Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# Makumbusho yapewe umuhimu wake katika uchotaji maarifa

KILA ifikapo, siku ya Mei 18 ya kila mwaka, huadhimishwa Siku ya Makumbusho Duniani.

Hiyo ni kutokana na umuhimu wa Makumbusho kwa kujifunza masuala mbalimbali kwa wanafunzi na wengineo. Umoja wa Mataifa uliridhia siku ya Mei 18 ya kila mwaka, iwe ni Siku ya Makumbusho Duniani.

Nchi zote duniani huitumia siku hiyo katika kutambua mchango wa Makumbusho kwa historia na maendeleo ya nchi zao.

Siku ya Makumbusho Duniani, mwaka huu yaliadhimishwa kitaifa katika Viwanja vya Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni Dar es Salaam.

Tukumbuke, Makumbusho ni nyenzo muhimu katika kutunza historia, mila, desturi, utamaduni na maendeleo ya nchi katika vipindi mbalimbali vya kimaendeleo.

Nchini, Makumbusho yamekuwa yakikosa kupewa umuhimu wa kipekee, hasa kwa taasisi mbalimbali za elimu na wananchi kwa ujumla, katika kuyatumia kama nyenzo muhimu ya kujifunza masuala mbalimbali.

Katika somo la Historia kuanzia shule za msingi hadi ngazi ya vyuo vikuu, Makumbusho ni moja ya vyanzo muhimu vya kupata taarifa za kihistoria.

Mfano hai wa Makumbusho yaliyopo nchini, ni pamoja na Makumbusho ya Taifa yaliyopo jijini Dar es Salaam; Bagamoyo, Pwani; Butiama, Mara; na Kalenga ya Bagamoyo.

Hapo pamejaa taarifa muhimu ambazo zinasaidia kupata uelewa wa mambo mengi. Kupitia Makumbusho, tunasoma taarifa za masuala mbalimbali yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kujifunza. Pia, yanamsaidia mtu kujifunza kwa kushuhudia kile anachotaka kujifunza.

Baada ya kusoma vitabu, mtu huweza kuthibitisha alichokisoma kwa kwenda Makumbusho kupata uhalisia.

Huko wapo wataalamu walioajiriwa na serikali kutoa ufafanuzi kwa wageni wanaotembelea Makumbusho, kwa ajili ya kujifunza.

Kwa maana hiyo, Makumbusho ni njia mojawapo ya kupata majibu ya maswali mengi yanayomtatiza mtafiti.

Hivyo, kutokana na umuhimu niliyoulezea kwa kifupi kuhusiana na taasisi au ofisi hiyo ya Makumbusho, nitoe rai yangu kwamba, hatuna budi kuwa na utamaduni wa kutembelea Makumbusho yaliyopo, kuongeza ufahamu na uelewa kuhusu nchi yetu na nyinginezo duniani.

Upo umuhimu wa serikali kuelimisha wananchi kuhusiana na upekee wa kutembelea Makumbusho yaliyopo katika maeneo mbalimbali nchini kujifunza.

Kama usemi ulivyo 'Elimu Haina Mwisho,' suala la kutembelea Makumbusho na kujifunza, daima lisionekane linawahusu wanafunzi pekee yao. La hasha!

Kila Mtanzania anapaswa kujihisi ana wajibu wa kutembelea Makumbusho akapate elimu.

Matangazo yanapaswa kuandaliwa na kusambazwa katika vyombo mbalimbali vya habari, kama vile runinga, redio na magazeti ili kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutembelea Makumbusho yaliyopo nchini.

Kama wananchi wataelimishwa vya kutosha, naamini watashiriki kutembelea Makumbusho na kuwa mabalozi wema wa kuwaelimisha wengine nao waone umuhimu kutembelea Makumbusho, ili wakafaidi hazina ya maarifa inayopatikana huko.

Aidha, kwa taasisi za elimu zenye wajibu wa kuandaa wahitimu wenye maarifa ya kutosha, ni vyema kuwepo mkazo wa kutembelea Makumbusho, ili wanafunzi wajifunze kwa kuona na kukata kiu ya maswali waliyoyaibua wakati wa lujifunza darasani.

Vilevile, ni njia ya kujifunza kwa vitendo. Wakufunzi na walimu wawaelekeze wanafunzi wao kuhusu umuhimu wa kutembelea Makumbusho, ili kuongezea maarifa kwa yale waliojifunza darasani na vitabuni.

Ikumbukwe, kutembelea Makumbusho ni njia mojawapo ya kufanya utalii wa ndani, unaomsaidia mwanafunzi kubadili mazingira ya kujifunza.

Hiyo inaibua ari kubwa ya wanafunzi kujifunza nje ya mazingira walioyazoea kila siku, shuleni au vyuoni.

Inafaa wanafunzi wakafikia hatua ya kuona umuhimu wa kubadili mazingira ya kujifunzia, pindi wanapotembelea Makumbusho.

Hata hivyo, inaacha changamoto ya fedha kwa ajili ya kugharamia safari za kwenda kujifunza katika Makumbusho, yaliyopo umbali mrefu kutoka katika taasisi ya elimu husika.

Ni jambo linalokatizwa na maandalizi ya awali, ili wazazi na walezi wa watoto wamudu gharama za kwenda kujifunza. Hiyo inasaidia kupatikana fedha za safari na kuwezesha mafanikio ya kujifunza.

Kwa taasisi za elimu zilizo karibu na Makumbusho, fedha za safari si kikwazo kwa safari, hivyo inatarajiwa taasisi zote za elimu zilizoko jirani na Makumbusho, watembelee mahali hapo kila mara na kujifunza kwa kina.

Wakati tunapoendelea kuadhimisha Siku ya Makumbusho, ni lazima tutambue umuhimu wake katika kukuza ufahamu, uelewa na maarifa kwa wananchi.

Ni lazima tutambue utajiri mkubwa wa maarifa unaopatikana mahali hapo, ambayo naamini ikitumika ipasavyo, tutajenga Taifa la watu wenye uelewa mzuri.

Tuyatumie Makumbusho kuchota maarifa yanayopatikana humo. Tafakari!

**●Mwandishi ni Mwalimu katika Shule ya Sekondari Mlali, iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Anapatikana kwa simu namba: (+255) 0764 666349.**

# Jukwaa la Tafakuri vigogo Dar es Salaam

**Na Romana Mallya**

JUKWAA la Tafakuri kuwakutanisha mabalozi zaidi ya 400 kutoka Afrika na nje ya Bara hilo, wastaafu na wanafunzi wa vyuo vikuu jijini Dar es Salaam ili kudadisi kwa pamoja uafrika na rasilimali kuwa ni urithi ulioachwa na waasisi wa mataifa hayo unaotakiwa kuenziwa.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Uhuru Media Group, Ernest Sungura, wakati akizungumzia kuhusu jukwaa hilo ambalo litafanyika kesho katika ukumbi wa Nkurumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kuanzia mchana.

Alisema jukwaa hilo litafanyika Jumamosi ambayo ni siku ya maadhimisho ya Afrika na kutakuwa na mdahalo, maonyesho ya urithi wa ukombozi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itagawa bure mkataba wa huduma kwa mteja.

"Jukwaa la Tafakuri limeandaliwa na Uhuru Media Group kwa ushirikiano wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano was Afrika Mashariki, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aliongeza: "Hili ni jukwaa la pili baada ya kutanguliwa na lile lililofanyika Machi 30, mwaka huu, tunatarajia kuyafanya majukwaa sita kwa mwaka kwa kuzunguka mikoa mbalimbali na baada ya muda tutavuka mipaka ya nchi yetu."

Sungura alisema kaulimbiu itakuwa ni "Uafrika wetu na Rasilimali za Bara Letu ni Urithi Wetu".

Alisema Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mstaafu, Prof. Rwekaza Mukandala, atatoa mada iliyolenga kuzungumzia dhana nzima ya siku ya Afrika ili vijana waelewe umuhimu wake.

Pia alisema Katibu Mkuu wa Wizara Maliasili na Utalii, Prof. Aldolf Mkenda, atazungumzia umuhimu wa mageuzi ya uchumi bara la Afrika.

"Tanzania imekuwa ni mfano bora Afrika, Rais John Magufuli anaonyesha mfano na njia kwa nchi nyingine bara hili namna ya kujikomboa kiuchumi na kwa msingi huo huo tunajitaji kuendeleza mijadala hiyo na kuja na mbinu za majadiliano ili tufanye mambo makubwa na Tanzania iwe mfano," alisema.

Pia alisema kutakuwa na kundi la wazee ambalo litaongozwa na Getrude Mongella, Balozi Christopher Liundi na Ummy Mafuga kutokea Zanzibar.

# Halotel yazindua huduma mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Halotel Tanzania, imekuja na huduma mpya ya mawasiliano iitwayo 'Mpango Mzima' ambayo itamuwezesha mtumiaji wa simu kupata unafuu katika huduma mbalimbali.

Mkurugenzi wa Halotel, Nguyen Van Son, alisema ujio wa huduma hiyo mpya na 'Kiganja' imelenga kumwezesha mtumiaji wa mtandao huo kutumia intaneti yenye kasi na ukubwa wa GB 5 bila kikomo.

Son alisema uanzishwaji wa huduma hiyo ni mwendelezo wa kampeni mbalimbali zinazoendelea kufanywa na kampuni hiyo katika kumrahisishia mteja kupata huduma bora.

Pia alisema lengo ni kumwezesha mtumiaji wa Halotel kupata huduma bora za mawasiliano zikiwamo za kutumia intaneti bila kikomo, kupiga simu mitandao yote na kutuma ujumbe mfupi wa maneno.

"Pamoja na intaneti hiyo mtumiaji wa mtandao huu ataweza kupiga simu kwenda mitandao yote bure kwa kila dakika 5 za kwanza pamoja na kuzawadiwa SMS 5000 atakazotumia kwa kipindi cha mwezi mzima," alieleza.

Son alisema huo ni mpango wa mapinduzi ya kimawasiliano wa Halotel kuwa karibu na kuwajali wateja wake kwa kutoa huduma bora.

"Kuanzishwa kwa Mpango Mzima kutamwezesha mteja wetu wa Halotel kutumia intaneti ya kasi kubwa, kupiga simu bila kikomo kwa mitandao yote bure kila dakika 5 za mwanzo, hivyo kumuondolea hofu ya simu kukatika kabla hajamaliza maongezi," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ili mteja aweze kunufaika na huduma hiyo mpya anapaswa kujiunga kwa kupiga 148*66# na kuchagua Mpango Mzima ambapo ataweza kujiunga na kuwa tayari kwa kuanza kufurahia unafuu huo.

Son alisema huduma ya Mpango Mzima ni mpya kuwahi kutolewa na mtandao mwingine wowote wa simu hapa nchini.

Pia alisema Halotel inaweza kuunganisha Optic Fiber zenye urefu wa zaidi ya kilomita 20,000 katika maeneo yenye miundombinu yake kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa data kwa maeneo mapya na hivyo kuwezesha kuwa chaguo la kwanza kwa wateja pale linapokuja suala la huduma za intaneti.

# Mradi hewa kabon maisha mapya wa

## ■Wafaidi mapato, huduma, hewa safi
## ■Binti masikini afurahia shule bure
## ■Wazazi kundi waangukia kuajiriwa

**Na Jenifer Julius**

NI umbali wa kilomita 300 kutoka mjini Arusha, mwendo wa saa tatu kwa basi binafsi, ndiko kunakopatikana kijiji cha Mongo wa Mono, katika wilaya ya Mbulu mkoani Arusha .

Katika kijiji hicho chenye mandhari ya kuvutia, iliyosheheni nakshi za kijani kibichi, inayokolezwa na sauti asilia kutoka kwa ndege wa kila aina. Hapo ndiko unakompata msichana Rachel Athumani, binti wa Kihadzabe, mwenye umri wa miaka 17.

Licha ya kutoka kwenye kijiji chenye hali duni ya maisha, baadhi ya familia zikiishi kwa mlo mmoja tu wa uhakika kwa siku, Rachel anaoneka na ni binti mwenye furaha wakati wote.

Ndani ya dakika 30 ya mazungumzo yake na Nipashe, majibu ya kisaikolojia yanaibua majibu ya yanayojiri kutoka tabasamu lake.

Licha ya kutoka katika familia masikini, Rachel, anajiona mwenye bahati kuwa mzaliwa katika kijiji cha Mongo wa Mono. Sababu kuu anataja ni kupata huduma zote muhimu za kijamii bure, hapo yakiwemo yanayomgusa moja kwa moja, elimu na matibabu.

Rachel aliyeko kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mangola, wilaya ya Karatu, analazimika kukaa bweninі, kwa sababu shule yao ipo mbali na binafsi hana wasiwasi, kwani kila kitu kinalipiwa kwa wakati.

Anataja siri ya kusoma kwake bila ya hofu ilhali wazazi wake ni wa kipato duni, ni kuwapo mradi wa upatikanaji hewa ya kaboni katika kijiji chake, unaoitwa Carbon Tanzania.

Huo ni mradi unaorejesha malipo ya huduma kwa wakazi, kama vile usafiri, kununua vifaa vya shule, pesa za matumizi pamoja na kugharamia matibabu yake.

"Ninaushukuru Mradi wa Carbon kwa kuwa umenifanya nisome kwa amani, bila ya kuwa na wasiwasi wowote kuhusu gharama za mahitaji yangu muhimu,"anasema Rachel.

Huyo ni mmoja wa wanafunzi 20 kutoka kijiji hicho wanaonufaika na mradi wa Kabon katika elimu. Wawili wao wapo kidato cha sita na watatu chuo kikuu.

Huo ni mradi unaolenga kutunza mazingira na unanufaisha wastani wa wanakijiji 5,900.

Mbali na kulipia gharama za shule, mradi huo umefanikisha ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Yaeda, ambayo hayajawahi kuongezwa tangu za awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi.

Paul Timotheo, ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Yaeda Chini, anasema wanapokea malipo kutoka mradi wa Carbon kila baada ya miezi sita kwa kuwa wanakijiji ndio walinzi wakuu wa misitu hiyo.

Anasema, fedha wanazopokea wanaziingiza kwenye miradi ya maendeleo kama vile kuingiza katika mfuko huduma za hospitali na elimu, pia majanga.

"Uwapo wa mifuko hii, huwezesha wanakijiji kupata huduma za kijamii bure mfano huduma za hospitali, ikiwamo matibabu na 'ambulance' (gari la wagonjwa) kutokana hospitali ipo mbali na kijiji," anasema Timotheo.

Anaendelea: "Mfano katika malipo ya kwanza tuliyopokea, tulitumia Sh. milioni 10 kujenga kituo cha polisi, ili kuongeza ulinzi na sh. milioni 17, tuliongeza majengo mawili ya madarasa katika Shule ya Msingi Yaeda, ambayo ilikuwa na madarsa sita tu wanayotumia darasa la kwanza hadi la saba".

Licha ya kuwapo huduma za kijamii, mradi huo uliopo katika vijiji vya Mongo wa Mono, YaedaChini na Domanga, umeinua kipato binafsi kwa baadhi ya wanakijiji, kwa kuwapatia ajira katika vitengo mbalimbali.

Ni takribani wanakijiji 42 katika Kata yaYaeda Chini wameajiriwa katika mradi huo, katika nafasi za utunzaji kumbukumbu na ulinzi, wakilipwa ujira wa Sh. 80,000 kwa mwezi.



Mikutano tofauti ya uongozi wa Mradi wa Carbon Tanzania, wakiwawasilishia wanakijiji faida itokanayo na mauzo ya hewa ya gesi ya kaboni, mikutano hiyo ilifanyika katika kijiji cha Mongo Wa Mono, katika Bonde la Yaeda. Fedha hizo hufanyiwa maamuzi na wanakijiji. **PICHA ZOTE: SOPHIE TREMBLAY NA MONGABAY.**






Pili Godo, ni mwanakijiji wa Domanga, anayefurahia uwapo wa Mradi wa Carbon katika kijiji hicho, kwa kuwa umempatia ajira ya utunzaji kumbukumbu inayomuwezesha kujenga nyumba ya kisasa.

"Ninaushukuru sana mradi huu, kwa sababu kupitia ajira niliyo nayo mimi na mume wangu, tumejenga nyumba ya kisasa na kuhama kutoka kwenye nyumba ya miti na nyasi tuliyokuwa tunaishia awali" anasema pili, ambaye hafichi uso uliojaa tabasamu.

Mkurugenzi wa Mradi wa Kaboni, Marc Baker, anaelekeza shukrani kwa wanakijiji wa Kata ya Yaeda Chini, kwa kushirikiana nao katika mradi huo wenye lengo kuu la kutunza mazingira, ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Anaongeza

# ni unavyowaletea windaji wa Mbulu




Wanakijiji wa Yaeda, wakifundishwa ramani ya maeneo kufanya shughuli zao za maendeleo na mipaka yao ya kazi, ikiwemo mradi wa Carbon Tanzania.

wango cha chuo kikuu.

"Tunashindwa kusomesha watoto wetu chuo kikuu kwa sababu hela tu nayopata ni ndogo na mradi hauhudumii vijana wetu walioenda shule,"analalama Chaka.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2012-2016 iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), asilimia 55 ya ardhi (sawa na kilomita za mraba148,000) ni misitu na asilimia 93 ya misitu huo ni mbao, huku asilimia saba zilizobaki ni aina nyingine, ikiwemo misitu ya pwani.

Akiongea katika Wiki ya Mkutano wa Mabadiliko ya Tabia Nchi kwa nchi za Afrika ukiofanyika jijini Accra, Ghana, mwakilishi kutoka Umoja wa Mataifa, BaloziLuis Alfonso De Alba, alisema kuwa dunia inatakiwa iweke nguvu kwenye utekelezaji wa sera za mabadiliko ya tabia nchi na katika kilele cha mkutano huo nchini Chile (COP 24) watajadili utekelezaji na ufuatiliaji wa utekekezaji na jinsi ya kusaidia mataifa yanayoendelea katika vita hii.




Ramani, inayoelekeza kijiji cha Mongo wa Mono, Mbulu. Chini, sehemu ya misitu inayohifadhi hewa ya kaboni. **PICHA: MTANDAO.**

kuwa kaboni inayozalishwa ni matokeo ya kazi nzuri ya utunzaji misitu inayofanywa na wanakijiji.

Anasema kazi yao wanashirikiana na serikali ya wilaya na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuwaelimisha wanakijiji juu ya faida zinazopatikana katika utunzaji mazingira na kijiji na wakiridhia, ndipo wanaanzisha mradi huo.

"Kaboni inayozalishwa tunaiuza kwa kampuni mbalimbali duniani, zinazohitaji kusafisha oksijeni na faida inayopatikana tunagawana na wanakijiji pamoja na kusaidia shughuli za maendeleo katika jamii husika" anasema Barker.

Jamii hiyo ya Wahadzabe ambao hutegemea uhai wa mazingira ili kuendeleza mila na desturi zao kama vile kuwinda, wamefanikiwa kuzuia ukataji misitu mara 20 na kuzuia miti 187,000 kukatwa katika kata hiyo.

**CHANGAMOTO**


Pamoja na kushukuru mradi wa kaboni, wanakijiji wanamalalamikia malipo wanayopata kuwa madogo na hayakidhi mahitaji yao ya familia.

Nange Chaka, anayefanya kazi ya ulinzi katika mradi wa kaboni, anausifu kuwa umebadilisha maisha yake kutoka ufugaji hadi mfanyakazi, lakini kipato chao bado ni kidogo.

Anawaomba wamiliki wa mradi kuwaongezea mshahara, ili waweze kumudu kuihudumua familia yao, hasa pale watoto wao wanapofikia ki-



## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 2 00)



Dondoo: Kulia

1. Waziri mkuu mwanamke U.K
4. Namna kitu kilivyo
7. Ngogwe
11.Kijiji Italia ilipopigwa na Ethiopia 12. Lalamika
15. Shetani
16. Idadi ya watumishi katika idara 18. Aminika
21. Eleza
23. Neno la mshangao
24. Msichana ambaye hajaolewa 25. Mwenyeji
27. Kiwanja 28. Dhamira
29. Mfugaji Arusha

Dondoo: Chini

1. Madini yaliyogunduliwa 1967
2. Mto wa pili kwa urefu duniani 3. Njiwa
5. Mashimo ya madini
6. Tunda la mkungu
8. Pesa ya China
9. Raruka kwa karatasi
10. Jiji la pili kwa ukubwa
13. Kipindi cha giza
14. Kaa kimya
17. Lilongwe ni mji wake mkuu 19. Lau, kama
20. Binadamu 22. Kati ya
23. Vamia 26. mchezo

## Jibu la Na: 1

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | A | K | A | T | I | | P | A | K | A |
| A | | A | | | | | | | A | |
| S | H | I | D | A | | U | G | U | Z | A |
| I | | M | A | N | A | | | R | A | I |
| W | A | U | N | G | W | A | N | A | | B |
| A | | | G | O | I | G | O | I | | I |
| S | | M | A | L | A | I | K | A | | K |
| I | | K | | A | | | I | | | A |
| | M | E | I | | M | A | A | N | A | |
| | | B | | | | | | I | | |
| M | T | E | K | E | L | E | Z | A | J | I |

MAKALA

# FAO: Dunia bila nyuki ni zahama kwa mustakabali wa chakula

SIKU ya nyuki duniani ni siku ambayo inatabainisha umuhimu wa nyuki na tishio linalowakabili viumbe hao.

Kutoweka kwao kutakuwa mtihani mkubwa kwa dunia, hususani kwa mustakabhali wa chakula, linasema Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO).

Kwa mujibu wa FAO, asilimia 75 ya matunda na mbogamboga visingekuwepo bila nyuki na ni bidhaa ambazo ni muhimu sana kwa uhakika wa chakula na bayoanuai ya dunia.

Hata hivyo, shirika hilo linasema nyuki wanakabiliwa na tishio kubwa dhidi ya wachavuaji wake zikiwemo aina zaidi ya 20,000 za nyuki, pia wadudu wengine na hata wanyama kama popo na nyani ambao pia wanaweza kufanya kazi ya kuchavusha.

Ofisa Kilimo na Mtaalamu wa Masuala ya Uchavuaji wa FAO, Abram Bicksler, anasema takwimu ziko bayana na kwamba hatua zisipochukuliwa sasa kudhibiti vyanzo vya tishio hilo, hali itakuwa mbaya zaidi katika siku za usoni.

Na hasa ukizingatia baadhi ya sehemu za Amerika na Ulaya, idadi ya nyuki imepungua sana.



Mizinga ya nyuki katika moja ya maeneo yanayofuga nyuki. **PICHA: MTANDAO**

**MFUGAJI NYUKI**

Eric Kanalstein ni Mfugaji wa nyuki anayefafanua zaidi kuhusu vyanzo vya tishio na mustakabali wa nyuki duniani akisema "Ni mchanganyiko wa sababu mbalimbali zote zikichangiwa na shughuli za binadamu...mabadiliko ya tabianchi ni sababu, kutopea kwa makazi ni sababu na matumizi ya kupindukia ya dawa za kuua wadudu ni sababu kubwa," anasema na kuongeza:

"Lakini pia magonjwa makubwa na wadudu vinaathiri wachavuaji... hivyo sababu hizi vikiwekwa kwa pamoja wachavuaji wetu wanakabiliwa na wakati mgumu."

Naye Mkurugenzi Mkuu wa FAO, Jose Graziano da Silva akisisitiza umuhimu wa nyuki anasema. "Zaidi ya asilimia 75 ya mazao ya chakula yanategemea kwa kiasi fulani uchavushaji wa nyuki matumizi na ubora," anasema na kuongeza:

"Kutokuwepo kwa nyuki na wachavushaji wengine kutaangamiza kahawa, Alimondi, tufaa, nyanya na kokoa kwa kutaja mazao machache tu ambayo yanategemea uchavushaji."

Anazihimiza nchi zote kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha wanalinda nyuki.

Mei 20, ilikuwa ni maadhimisho ya Pili ya kimataifa ya siku ya nyuki duniani baada ya kupitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa mwaka 2017 na kuanza kuadhimishwa rasmi Mei 20 mwaka jana.

**MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU (SDGs)**

Mchango wa nyuki ni muhimu sana katika juhudi za dunia za kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs).

Hiyo ni kauli inayotolewa katika siku ya maadhimisho ya nyuki duniani na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Amina Mohamed.

Akizungumza kwenye hafla maalumu ya ya maadhimisho hayo, Amina amesema hakuna viumbe duniani wanaofanya kazi sana kama nyuki na hasa nyuki wadogo na wachavushaji wengine katika kuhakikisha robo tatu ya mazao ya chakula duniani yanachavushwa.

Anaongeza kuwa na mazao ambayo yameshachavushwa vyema kunadhihirika kutokana na ladha nzuri na kuwa na virutibisho muhimu, muonekano mzuri na kudumu kwa muda mrefu.

**MCHANGO WA NYUKI**

Zaidi ya lishe anasema mchango wa nyuki pia ni mkubwa katika masuala ya uchumi kwani:

"Ufugaji wa nyuki na mazao yake kuanzia asali, nta na masega ni vyanzo vikubwa vya mapato hususan kwa watu waishio vijijini...na hilo ni la msingi sana kwetu hasa katika kutokomeza umasikini na njaa," anasema Amina.

**UKWELI HALISI KUHUSU NYUKI**

Naibu Katibu Mkuu huyo anasema utafiti mmoja wa kimataifa unakadiria kuwa uzalishaji wa chakula kimataifa wa kila mwaka ambao unategemea uchavushaji una thamani ya dola bilioni 500 au (nusu trilioni), kiasi ambacho ni kikubwa katika kuchangia maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, anasema licha ya mchango huo idadi ya nyuki na wachavushaji wengine imepungua kwa kiasi kikubwa.

Anabainisha kuwa kilimo cha kupindukia kisichozingatia mpangilio na dawa za kuua wadudu vinawaweka nyuki katika hatari kubwa.

Anasema nyuki wanakabiliwa na magonjwa mapya ya wadudu na mabadiliko ya tabianchi yamekuwa tishio kubwa kwa viumbe hawa.

**AMINA ANASISITIZA:**

"Kupungua na kutoweka kwa nyuki na wadudu wengine wa porini kuna athari kubwa kwa mfumo wa maisha ya kimataifa na mustakabali wa binadamu...juhudi mbalimbali za haraka zinahitajika kuwalinda nyuki porini, katika kilimo na katika makazi ya mijini."

Anahimiza kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali, jumuiya za wafuga nyuki, mashirika ya utafiti na wanazuoni wana jukumu kubwa katika hili.

Na mwisho anatoa wito kwa dunia na kwa kila mtu kwamba "Suala la kutoweka kwa nyuki sio utani ni la hatari na maadhimisho haya yamekuja katika wakati muafaka... tunadhamiria kuivalia njuga changamoto hii kote duniani," anaongeza:

"Hivyo tushirikiane na kufanya kazi pamoja kuhakikisha kwamba wadudu hawa wanaochapa kazi kuliko kawaida wanaweza kuishi ili mfumo wa maisha na binadamu wanaowategemea waweze kufanya hivyo pia katika kizazi cha leo na vijavyo."

**HATUA ZA KUCHUKUA KULINDA NYUKI**

Kwa mujibu wa FAO, kuna mambo sita ya kuzingatia ili kuwaenzi na kunusuru maisha ya nyuki kutokana na faida zao kwetu.

WANABORESHA LISHE YETU

Nyuki wanaboresha lishe yetu kwa kutoa virutubisho muhimu vinavyoimarisha mazao kama matunda, mbogamboga, mbegu, jamii ya njugu, kahawa, kokoa na almondi na mafuta. Bila nyuki mazao haya yatatoweka.

Ili kulipa fadhila kwa wadudu hawa, wanabidi kupewa chakula wapendacho kwa kupanda mazao asilia kwenye bustani, kwani nyuki na bustani ni kama pete na chanda, wanahusiana na kutegemeana.

**NYUKI WANATUPA ASALI**

Je, wafahamu kuwa katika zaidi ya aina 20,000 za nyuki, ni aina 7 tu ndizo za nyuki wanaotoa asali?

Na aina ya nyuki ya Western ndio huzalisha asali nyingi zaidi sawa na tani milioni 1.6 kila mwaka?

Bidhaa hii ya asili ni tamu na pia ni dawa dhidi ya bakteria na kwa vidonda...ni chanzo kikubwa cha mapato kwa wafugaji na wakulima vijijini.

Hivyo basi ni vyema kununua asali ghafi kutoka kwa wakulima kwani wengi ndio wanaozingatia ufugaji endelevu wa asili, lakini pia ni kuwasaidia wakulima kwa kununua asali, nta, na bidhaa zingine zitokanazo na nyuki.

**WANA MAADILI BORA ZAIDI YA KAZI**

Nyuki mmoja wa asali anaweza kutembelea takribani maua 7000 kwa siku na inahitaji maua milioni 4 ili kuzalisha kilo moja ya asali.

Na nyuki hawa hufanyakazi kama timu bila kuchoka ili kusaidia kuandaa masega tayari kwa kuzalisha asali.

Kufanya kazi bila kuchoka kulichangia kuanzishwa msemo wa "unafanya kazi kama nyuki"

Basi kwa kazi hiyo kubwa ni vyema kuwaenzi nyuki hawa kwa kuwawekea chombo cha maji, kwani baada ya kibarua hicho kigumu wanahitaji kunywa maji. Ni njia nzuri ya kuwafanya wapumzike.

**LADHA KATIKA CHAKULA CHETU**

Mazao yaliyochavushwa vyema hutoa chakula kingi, kinachofanana na matunda na mbogamboga zenye ladha nzuri.

Mfano matufaa ambayo yameharibika inamaanisha hayakuchavushwa vizuri.

Ili kuwalinda viumbe hawa ni kuepuka matumizi ya dawa za kuulia wadudu, dawa za fangasi, au dawa zingine za kupulizia kwenye bustani, kwani dawa hizi zinaweza kuwaua wavachuaji wetu na kutia sumu kwenye masega ya nyuki ambayo hatimaye yanaweza kuathiri hata asali yenyewe. Jaribu kutumia njia za asili kukabiliana na wadudu.

**WANAONGEZA UZALISHAJI NA UHAKIKA WA CHAKULA**

Moja ya tafiti ambako uchavuaji ulikuwa unafanyika kwa mpangilio katika kundi dogo la wakulima, mazao yaliongezeka kwa asilimia 24.

Hivyo nyuki na wachavuaji wengine wanaboresha maisha ya wakulima wadogo wadogo bilioni mbili duniani kote ambao wanasaidia kuhakikisha uhakika wa chakula.

La kufanya sasa ni kutengeneza mazingira mazuri ya nyuki ili kuhakikisha uchavuaji bora na endelevu kwa nyuki.

Inabidi kuhakikisha mazingira yanaachwa kama ya shamba katika hali ya uasilia.

NYUKI HULINDA BAYOANUAI

Uchavuaji ni moja ya mchakato muhimu wa kiasili ambao huchangia katika bayoanuai ya dunia, unatusaidia kuzalisha aina mbalimbali za mimea ambayo asilimia kubwa ni ya chakula.

Asilimia 90 ya miti ya maua kote duniani inategemea uchavuaji kwa ajili ya kuzaliana.

**IMEKUSANYWA KUTOKA UN**

## HABARI KIMATAIFA

# Waziri Mkuu Uingereza kujiuzulu Juni

**LONDON, Uingereza**

HATIMAYE Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, ametangaza rasmi kujiuzulu huku akisema kuwa ataondoka rasmi katika nafasi ya uongozi wa chama cha Conservative ifikapo Juni 7, mwaka huu.

Hatua hiyo inamuweka May kwenye rekodi ya Mawaziri Wakuu wa Uingereza walioongoza kwa muda mfupi tangu mwaka 1900, ambapo aliingia madarakani kuanzia 2016 hadi mwaka huu, akiwa madarakani kwa miaka miwili na siku 315.

Andrew Bonar Law aliongoza kuanzia mwaka 1922 hadi 1923 ikiwa ni muda wa siku 209, Alec Douglas kuanzia mwaka 1963 hadi 1964 aliongoza kwa siku 364, Anthony Eden aliongoza kuanzia mwaka 1955 hadi 1957 aliongoza kwa mwaka mmoja na siku 279.

Wengine ni Henry Campbell-Bennerman aliongoza kuanzia mwaka 1905 hadi 1908, ikiwa ni miaka miwili na siku 122, Gordon Brown aliongoza kuanzia mwaka 2007 hadi 2010 ikiwa ni miaka miwili na siku 319.

May ametoa fursa ya kuidhinishwa kwa mchakato wa kuchaguliwa kwa Waziri Mkuu mpya wa Uingereza.

Hali hiyo imetokea baada ya kushindwa kupata uungwaji mkono wa wabunge katika mpango wake wa kutaka Uingereza kujiondoa kutoka kwenye Umoja wa Ulaya, Brexit.

"Nitaiachia kazi hii hivi karibuni, imekuwa ni fahari kubwa kuishikilia nafasi ya Waziri Mkuu wa kwanza mwanamke, bila shaka sitakuwa wa mwisho. Naondoka bila nia mbaya, ila shukrani kubwa ya kuweza kuihudumia nchi ninayoipenda," alisema May.

Hata hivyo, May ataikaimu nafasi hiyo ya kiongozi wa chama cha Conservative hadi pale kiongozi mpya atakapochaguliwa hatua ambayo inatarajiwa kuchukua wiki kadhaa.

Baada ya hatua hiyo, Kiongozi mpya atachukua nafasi ya Waziri Mkuu na hakutakuwa na haja ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

Mbunge yeyote wa chama cha Conservative anaweza kuiwania nafasi hiyo ya uongozi wa chama, lakini mtu anayepewa nafasi wa kwanza kwa sasa ni Boris Johnson, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani Uingereza.



Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, akibubujikwa na machozi wakati akisoma risala ya kujiuzulu nafasi yake. **PICHA: REUTERS**

May anaachia ngazi akiwa hajayatimiza malengo aliyokuwa ameapa kuyatimiza wakati alipokuwa anachukua nafasi hiyo ya Waziri Mkuu.

Wakati anachukua kiti cha Uwaziri Mkuu, May alisema kuwa angehakikisha kuwa Uingereza imejiondoa kutoka Umoja wa Ulaya na atapatanisha pande zilizogawanyika kutokana na suala hilo la Brexit.

Kuondoka kwake kutauzidisha mzozo wa Brexit kwa kuwa kuna uwezekano kuwa kiongozi mpya atataka makubaliano mazuri zaidi ya kujiondoa, jambo ambalo litazua mkwaruzano na Umoja wa Ulaya na hata uchaguzi wa mapema wa bunge.

Umoja wa Ulaya tayari umeshaeleza kuwa hautafanya majadiliano mengine zaidi kuhusiana na maelewano waliyoafikiana na May mwezi Novemba.

May anang'atuka madarakani akiwa ameiacha Uingereza ikiwa imegawanyika sehemu kubwa na wanasiasa ambao hawajui ni kwa njia gani, lini waifanikishe dhumuni lao la kujitoa Umoja wa Ulaya.

Kujiuzulu kwa May kumetokana na shinikizo kuwa kubwa kutoka kwa chama chake baada ya kushindwa kuiongoza Uingereza katika Brexit kwa muda uliokuwa umepangiwa.

Mamlaka yake yalikuwa yanaonekana kupungua kadri muda ulivyokuwa ukisonga na Alhamis May alichelewesha kuwasilisha mswada wake wa Brexit, jambo ambalo lingekuwa jaribio lake la nne kutaka kupata idhini ya bunge kuhusiana na makubaliano yake na Umoja wa Ulaya.

Uingereza inatarajiwa kuondoka kwenye Umoja wa Ulaya Oktoba 31 lakini hilo litafanyika iwapo tu bunge litaidhinisha maelewano ya makubaliano.

***DW***

# WHO: Hakuna tena Malaria Algeria, Argentina

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesema Algeria na Argentina zimethibitishwa na kutambulika rasmi kuwa zimetokomeza ugonjwa wa malaria.

Hatua hii inamaanisha katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, hakujaripotiwa hata tukio moja la mgonjwa wa malaria katika nchi hizo.

Malaria ni ugonjwa unaotokana na kuumwa na mbu umesalia kuwa ni moja ya magonjwa yanayoongoza kwa vifo duniani.

Inakadiriwa kuwa mwaka 2017 pekee kulikuwa na matukio Milioni 219 na vifo zaidi ya 400,000 vya malaria, huku asilimia karibu 60 ya vifo hivyo vikiwa vya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano.

Algeria ni nchi ya pili katika ukanda wa Afrika kutambuliwa rasmi na WHO kama imetokomeza malaria baada ya Mauritius ambayo ilithibitishwa rasmi mwaka 1973.

***RFI***

**Malaria ni ugonjwa unaotokana na kuumwa na mbu umesalia kuwa ni moja ya magonjwa yanayoongoza kwa vifo duniani.**

# Mutharika aongoza matokeo uchaguzi mkuu

**LILONGWE, Malawi**

RAIS wa Malawi, Peter Mutharika, anaongoza matokeo ya awali ya uchaguzi mkuu kwa asilimia 40.44 ya kura zote zilizopigwa.

Hadi jana asilimia 75 ya kura zilizopigwa zilikuwa zimehesabiwa kulingana na tume ya uchaguzi nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Tume ya Uchaguzi, Lazarus Chakwera, ambaye anaongoza chama cha upinzani cha Malawi Congress Party amepata kura asilimia 35.34 huku Makamu wa Rais, Saulos Chilima amejipatia asilimia 18.35.

Alhamisi Chakwera alikuwa anaongoza baada ya chama chake cha MCP kujipatia kura 533,217 ambayo ni sawa na asilimia 37.65.

Alikuwa anafuatiwa kwa karibu na Rais Peter Mutharika ambaye alikuwa amepatia kura 524,247 ikiwa ni asilimia 37.1 huku Makamu wa Rais Saulos Chilima wa United Transformation Movement akiwa wa tatu akiwa amepata kura 293,978 ambayo ni asilimia 20.76.

Akizungumza na waandishi wa habari, Chakwera alisema kuwa matokeo hayo ya mapema yalimpatia matumaini ya kushinda katika uchaguzi huo.

Hata hivyo, aliongezea kwamba kulikuwa na jaribio la baadhi ya watu wasiojulikana kuingilia matokeo ya uchaguzi huo huku akiapa kwamba hatokubali udanganyifu wowote kutokea.

Lakini tume ya uchaguzi nchini humo imetoa wito wa kuwapo kwa utulivu ikisisitiza kuwa ndiyo yenye uwezo wa kutangaza matokeo hayo.

Uchaguzi huo umekumbwa na ushindani wa karibu kati ya Rais Peter Mutharika, Makamu wake Saulos Chilima na Chakwera ambaye anakiongoza chama cha Malawi Congress party.

Katika uchaguzi wa mwaka 2014, Chakwera alipoteza kwa karibu dhidi ya Rais Mutharika na alishindwa kupinga matokeo ya uchaguzi huo mahakamani.

Tume ya Uchaguzi imebakiza siku nne tu kutangaza matokeo ya uchaguzi huo, hata hivyo imekiri kwamba inakabiliwa na changamoto za kiufundi katika utangazaji wa matokeo hayo,lakini imesema kuwa ina imani itatoa matokeo yalio huru na haki.

Hii ni mara ya kwanza kura kujumlishwa na kutumwa kwa njia ya kielektroniki nchini Malawi.

Zaidi ya wapiga kura milioni saba walipiga kura kumchagua rais, wabunge na madiwani Mei 21 katika uchaguzi ambao hauwezi kutabirika katika historia ya nchi hiyo.

***BBC***

# HADITHI

# Jumba Jekundu-2

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

KWENYE makutano ya barabara inayotoka Ubungo kwenda Bamaga na ile ya kwenda Sinza Darajani, sehemu za Sinza kijiweni kuna jengo moja la ghorofa nne.

Mbele kuna maandishi makubwa yanayosomeka 'Blue Star'. Ni mmoja ya hoteli za kisasa kabisa zilizoota kama uyoga, kwenye zama hizi za uwekezaji.

Humo ndani kunapatikana kila kitu. Ilikuwa ni saa 1:00 usiku wakati magari kutoka pande zote za jiji la Dar es Salaam, yalipokuwa yakipaki.

Vijana, wasichana, wazee na wanawake wa makamo walionekana wakimiminika kuingia kwenye hoteli hiyo.

Watu walishindana kuvaa utafikiri kulikuwa na mashindano ya mavazi ya dunia. Waliovaa nguo nzuri na za gharama walishindana na wenzao, na waliovaa nguo fupi zenye kuonyesha maungo yao, nao walionekana kushindana, kwani kila utakayemuona alionekana kuvaa fupi zaidi kuliko mwenzake. Mchanganyiko wa manukato kwenye eneo hilo uliosababisha kuwa na harufu ya kupendeza, kwani warembo walishindana kwa manukato. Kulikuwa na wenye pafyumu za Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, Uarabuni na nchi nyingine ambazo ni wataalam wa kutengeneza pafyumu za uhakika.

Watu wengi walioingia kwenye hoteli hiyo, waliishia kwenye ghorofa ya pili ambapo kila wiki, Jumamosi na Jumapili kunakuwa na disco la kukata na shoka.

Ni sehemu ambayo vijana kutoka sehemu mbalimbali kujumuika kwa ajili ya kufurahi na wenzao, huku watu wazima waliogoma kuzeeka na wenye pesa wakienda nao kula kuku kwa mrija.

Siku hiyo, Kadili na rafiki yake Meze walikuwa ni sehemu ya watu waliofika kwenye hoteli hiyo kwa ajili ya kufurahi na kukumbushia enzi zao wakiwa nado wanasoma sekondari na sasa mmoja yupo Chuo cha Teknolojia, wenzake akiuza duka la mjomba wake.

Eneo hilo la ghorofa mbili liligawanywa sehemu tatu. Moja ikiwa ni ya watu kuburudika kwa kunywa vinywaji wabavyojisikia, lakini ya pili ni ya watu ambao wao mbali na kunywa, lakini wana mapenzi na mchezo wa soka, hivyo sehemu hiyo ilitengwa kwa ajili ya kuangalia mpira wa miguu, hasa Ligi mbalimbali za Soka Duniani.




Sehemu ya tatu ilikuwa ni 'dance floor'. Ilitengwa kama sehemu ya kucheza muziki. Kwa muda huu sehemu ya kuchezea muziki haikuwa na watu wengi. Sehemu ambayo watu walikuwa wamelundikana ni ile ya kupata vinywaji. Mara nyingi sehemu hii huwa ya kwanza na watu wanapopata nishai, ndipo wanapohamia kwenye 'dance floor'.

Ni Kadili na Meze tu ndiyo waliokaa kwenye meza yao wakiwa wanaume watupu. Meza zote ama kulikuwa na mwanaume mmoja na mwanamke mmoja, au zaidi. Labda kwa sababu wao hawakuwa na cha ziada zaidi ya kwenda kucheza disco tu.

Kila mmoja alikuwa na pesa ya bia tatu tu, hivyo waliagiza kila mtu moja moja, huku kwa muda mrefu kazi yao ikiwa ni kuangalia vituko vya wanywaji wengine ambao tayari walishaanza kulewa.

Ilipofika saa nne usiku, akili za watu wengi ndani mle zilibadilika. Sasa kila mtu alikuwa na uwezo wa kufanya anavyojua. Wengi walikuwa wamelewa. Wengi sasa walihama kwenye sehemu ya kunywea na kuhamia kwenye 'dance floor.'

Ni wakati ambao Kadili na Meze walikuwa wanausubiri kwa hamu. Walijitosa kucheza muziki. Walikuwa wakicheza kama 'patna'. Na ni wao tu walikuwa wanaume watupu kucheza hivyo. Wengi walicheza mwanaume na mwanamke.

Kadili na Meze kila mmoja alikuwa anataka kumuonyesha mwenzake kuwa bado wapo kwenye kucheza muziki. Wakumbuka wakati huo walipokuwa wakicheza tangu shule ya msingi, sekondari na hata kwenye sherehe mbalimbali mtaani kwao walipokuwa wakitoa fora wao wawili na kujipatia pesa za kutunzwa na zawadi mbalimbali.

Dj, aliweka ngoma ya Korede Bello iitwayo 'Godwin'. Ni ngoma iliyowafurahisha wengi ukumbini humo, kila mmoja akicheza kwa kadri alivyoona kuwa anaweza kucheza.

Kadili alifanikiwa kucheza kwa kiwango cha juu ngoma hiyo, ingawa mwenyewe hakudhani kama alifika kwenye kiwango kinachotakiwa.

Kwa upande wa pili kuna mrembo mmoja alifanikiwa kumuona na kushangazwa na ustadi wa uchezaji wa Kadili kwenye ngoma hiyo.

Ngoma ilipomalizika, wengi walitaka Dj, airudie. Wakati inaanza tu, Kadili alihisi mkono wake kushikwa na kitu laini kama sufi.

Haikuwa sufi. Alipogeuka tu alijikuta kama amepigwa na shoti ya umeme. Macho yake alikutana ana kwa ana na kitu kama malaika aliyeshushwa mbinguni mara moja kwa kazi maalum.

Alikuwa msichana mrembo zaidi ya warembo. Mrefu mwembamba, mwenye mwili mororo, maji ya kunde, mwenye macho malegevu, nywele zake zilikuwa ndefu mpaka ngongoni, ingawa kwa Wabantu, hizo zitakuwa si halisi.

Pamoja na wembemba wake, lakini kiunoni alikatika na kuacha shepu iliyotenganisha yeye na wasichana wengine wembamba.

Macho malegevu yaliyokuwa yakisihi, yalitazama Kadili. Mdomo wake ulikuwa ni kama umefungwa waya au mnyororo. Hakuweza kuinua mdomo na kutamka neno lolote. 'Si habari zako mrembo wala, kipi unahitaji bibie.' Kwa ujumla alipigwa butwaa.

Mrembo hakuongea neno lolote, alitabasamu na kumuashiria kwa mikono kuwa acheze naye.

Meze alijiweka pembeni akiwaachia wenye meno watafune. Walichokishuhudia Meze na yule mrembo ni kwamba Kadili hakuweza kucheza kwa umahiri kama alivyofanya mwanzo. Ni kwa sababu ya mshtuko alioupata juu ya mrembo yule ambaye hakumfahamu.

"Cheza kama ulivyokuwa ukicheza mwanzo." Ilikuwa ni sauti nyororo na ya kubembeleza kutoka kwa binti yule.

Kadili alijitahidi kadri ya uwezo wake, ingawa hakuwa na uhakika kama alicheza vema kama mwanzo.

Baada ya ngoma hiyo kumalizika, ukaunganishwa na wimbo wa 'My Love', songi lililopigwa na Westlife.

Ulikuwa ni wimbo wa kukumbatiana baina ya mtu na mpenzi wake. Mikono ya Kadili ilikuwa na kigugumizi, lakini mrembo alimkumbatia na mkono wake kumshika Kadili kikamilifu hadi ngoma ilipomalizika.

Kabla ngoma ya tatu haijawekwa, watu wawili wenye miili mikubwa iliyojengeka walifika aliposimama Kadili na yule mrembo alisiyejulikana na kumuashiria kwa ishara kuwa muda umekwisha.

Haraka, bila kuaga, mrembo huyo aliondoka na hakuonekana tena kwenye kundi la watu waliokuwa wakicheza muziki. Ilikuwa tayari saa tano na dakika ishirini, huku disco likitarajiwa kumalizika saa sita usiku.

Baada ya tukio lile, Kadili hakuwa tena na nguvu ya kucheza muziki. Alirejea kwenye kiti chake kule walikokuwa wakinywa, huku akiwaza kilichomtokea dakika kadhaa zilizopita kuwa ni tukio halisi au ni ndoto?

Harufu ya pafyumu ya gharama ya hali ya juu ya mrembo yule ilibaki kwenye fulana yake aliyovaa, ikimthibitishia kuwa tukio lile ni la kweli.

"Msichana wa wapi yule? Mbona ni mzuri sana?' Alijiuliza. "Na kwa nini alinifuata mimi na kuniomba tucheze naye na si wanaume wengine waliojaa kwenye kumbi, tena wa hali na hadhi ya juu kuliko mimi?"

"Kadili twende nyumbani, naona hauko vizuri sasa." Meze alimshtua mwenzake kwa namna ya utani.

"Mzee Baba naona mambo yako safi, umebambiwa na mtoto wa kishua, mwanangu sikuwezi." Bado Meze alikuwa akizidi kumkoroga mwenzake.

Jinsi alivyo, gharama ya nguo zake, uvaaji na vipodozi alivyokuwa amejipodoa, ni kweli kabisa alionekana si aina ya wasichana wanaokwenda kwenye kumbi za starehe kutafuta mabwana. Hilo pia lilikuwa kwenye mawazo ya Kadili.

Msichana anayetafuta bwana asingeweza kumfuata yeye alionekana kuvaa nguo za hali ya chini, wakati kulikuwa na mashefa kibao waliojazana ukumbini mle ambao kwa jinsi alivyo na alivyovaa angefanana nao kihadhi.

"Msichana wa aina gani? jini?" Alizidi kujiuliza.

*Itaendelea Jumamosi*

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

### NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836


NIPASHE
NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu : +255 26 2324455
Fax: 255 26 2323233
Barua pepe : ps@mow.go.tz

Mtaa wa Kaunda
S.L.P 512,
MOSHI
24/05/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 25/05/2019 Kampuni ya Musa holding itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Boma ng'ombe - Hai – Moshi hadi Holili Rombo gari lenye namba za usajili T277ALQ.
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu - 9.7
   Upana - 3.0
   Kimo - 3.0
3. NJia itakayotumika kurudi ni Holili Rombo Moshi mpaka Bomang'ombe - Hai

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115247502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
24/05/2019


**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAPILI** tarehe **26/05/2019** kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MONDULI kuelekea SINGIDA gari hilo lenye namba za usajili: **T188APK, T741 CPB, T329BKM.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 8.6
   Upana –mita 3.0
   Kimo – mita 4
3. Njia itakayotumika **MONDULI hadi SINGIDA** kupitia BABATI ROAD gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115247402

### CHETI KIMEPOTEA



**BRIGHTONE MANGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0175-504** kilichotolewa na **SALESIAN SEMINARY** mwaka 1993.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/KIJ/RB/25571/2019.**

115247202

### KUPOTELEWA NA KADI YA TRAILER

**IBRAHIM SHABANI NGUA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trailer yenye namba za usajili **T 784 CKA.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**OB/RB/4503/2019.**

115246702


Kwa Habari
Motomoto
usikose
Gazeti lako

KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO
Tupigie 0767 223311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?
Nipashe
NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# POCHETTINO SASA KUBAKI ENGLAND

**LONDON, England**

KOCHA Mauricio Pochettino, ameshawishiwa kubaki ndani ya kikosi cha Tottenham na kusema kuwa ni miongoni mwa timu bora ambayo inashiriki ligi bora duniani.

Pochettino alinukuliwa akisema kwamba mchezo wake wa mwisho utakuwa dhidi ya Liverpool ambao utakuwa ni wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hivyo kama wasingemsajili mchezaji mmoja kwa gharama kubwa kwenye dirisha la usajili angebwaga manyanga.

Hata hivyo ametengua kauli yake hiyo kwa kuwa bado anaona timu hiyo ya Spurs ina maono makubwa na kuelezea namna anavyoiona ikiwa ni miongoni mwa timu bora duniani.

"Leo Tottenham ni kwa ajili yangu, ni klabu bora ndani ya ulimwengu wa michezo hasa ukizungumzia upande wa miundombinu, maeneo ya kujifunzia, uwanja mzuri ambao ni bora hakuna klabu bora kama hii.

"Pia ndani ya Uingereza hakuna mji mzuri zaidi ya Liverpool, na ligi bora duniani ni Ligi Kuu England na pia ni ligi ngumu miongoni mwa ligi ambazo zimewahi kutokea, hivyo malengo yangu ni kuifanya Tottenham kuwa timu bora duniani," amesema.





# WENGER: NARUDI KWENYE SOKA

**LONDON, England**

KOCHA Arsene Wenger amebainisha kuwa anaweza kurudi kwenye uongozi, lakini atarudi kwa staili tofauti kabisa.

Gwiji huyo wa zamani wa Arsenal aliamua kustaafu baada ya kukaa kwa washikabunduki hao kwa kipindi cha miaka 22 na bado hajarudi tena kwenye uongozi, licha ya kuhusishwa na kabu kadhaa za Ulaya.

Akizungumza na BBC Sport, Wenger amesema kwamba, wakati wowote anaweza kurudi kwenye uongozi wa soka.

"Kama unavyoweza kuona kwenye soka, naweza kurudi wakati wowote, ingawa sijajua muda muafaka bado.

"Nilifikiria kwamba ningerudi katika uongozi haraka iwezekanavyo, lakini mambo yamekwenda tofauti. Lakini kwa sasa nakaribia kurudi."

Kwa kipindi cha miaka 22 aliyokaa na Arsenal, Wenger aliiwezesha kutwaa mataji ya Ligi Kuu England, FA pamoja na lile la Kombe la Ligi.

# Liverpool kusajili mshambuliaji tu

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL wataingia sokoni kusaka washambuliaji wapya kwenye dirisha hili la majira ya kiangazi huko Ulaya.

Daniel Sturridge anaondoka na kutokana na hilo Klopp ana majina ya washambuliaji 12 ambao anawafuatilia mmoja baada ya mwingine na kwenye dirisha hili la usajili kuna mmoja wapo atatua Anfield kufanya mambo.

Hata hivyo, Kocha Jurgen Klopp mpango wake ni hataki kutumia pesa nyingi sana katika kuboresha safu yake ya ushambuliaji baada ya kuwa na wakali wengine kama Divock Origi na Rhian Brewster, ambao wanaongezea nguvu kwenye ile fowadi ya Sadio Mane, Roberto Firmino na Mohamed Salah.

Daniel Sturridge anaondoka kutokana na hilo Klopp ana majina ya washambuliaji 12 ambao anawafuatilia mmoja baada ya mwingine na kwenye dirisha hili la usajili kuna mmoja hapo atatua Anfield kufanya mambo. Staa wa zamani wa Chelsea ambaye aliendа kwa mkopo Ajax na Vitesse kabla ya kunaswa jumla na Lyon. Winga Traore ni balaa anapokuwa uwanjani huku kasi yake ndicho kitu kinachowavutia Liverpool na kuhitaji saini yake. Umri wake ndio kwanza miaka 23.






# MBAPPE, NEYMAR SASA WASUBIRIWA MADRID

**MADRID, Hispania**

MIAMBA ya soka la Hispania, Real Madrid, inasubiri uamuzi ya nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe au Neymar kuhusu uwezekano wa kujiunga na klabu hiyo msimu huu.

Gazeti maarufu Hispania, AS limechapisha taarifa ya mastaa hao, yenye kichwa cha habari kuwa ni Mbappe au Neymar waliokwenye mtego wa Florentino (Perez).

Taarifa hiyo iliendelea, "Unasubiriwa muongozo wa mmoja wapo au wengine wanaweza kuingia."

Mbappe ambaye alitwaa tuzo ya mchezo bora wa mwaka wa Ligi Kuu Ufaransa 'Ligue 1' maneno yake aliyosema Jumapili, baada ya kutwaa tuzo hiyo, yameanza kutofasiriwa kuwa huenda yuko mbioni kuondoka.

"Kuna mambo ambayo hayakwenda sawa (huu msimu), lakini ndio maisha ya mpira yalivyo, kikubwa tumeweza kuendelea kutetea ubingwa wa Ligi.

"Niseme asante kwa kocha na kwa klabu tena. Kitu muhimu kwangu ni kwamba hii ni hatua ya kwanza au ya pili kupiga kwenye uchezaji wangu soka," alisema Mbappe.

# Gwiji Arsenal ataka Ozil auzwe

**LONDON, England**

GWIJI wa zamani wa Arsenal, Ian Wright, amewataka mabosi wa klabu hiyo kuachana na mpango wa kumuuza kiungo wao mchezeshaji, Mesut Ozil ambaye inadaiwa hatakiwi na Kocha, Unai Emery.

Wright anaamini Arsenal itakuwa inafanya makosa makubwa kumwondoa staa huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani ambaye anadai bado anabakia kuwa mchezaji mbunifu zaidi katika kikosi cha Arsenal.



Ozil amecheza Arsenal kwa miaka sita lakini bado ameshindwa kuwashawishi mashabiki wa Arsenal wampende huku wengi wakiamini staa huyo ni mvivu licha ya kupendwa na kocha aliyepita, Arsene Wenger.

Amekuwa akikosa mwendelezo wa ubora na mara nyingi ameshindwa kutamba katika mechi kubwa huku Machi mwaka jana, kocha aliyepita, Wenger akimpatia mkataba mnono ambao unamfanya alipwe mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

Inadaiwa Arsenal imekuwa ikisaka timu ya kumuuza Ozil katika dirisha hili kwa ajili ya kuunda kikosi chake upya, lakini Wright ambaye kwa sasa ni mchambuzi wa soka England amekuwa na mawazo tofauti.

"Sina tatizo na kile ambacho Mesut Ozil anaingiza katika mshahara wake kwa sababu mwisho wa siku unahitaji wachezaji wanaomzunguka ambao pia watasababisha na yeye awe bora," aliongeza staa huyo wa zamani wa England.

Ingawa yeye na wenzake wana nafasi ya kutwaa ubingwa wa Europa katika pambano la fainali za michuano hiyo jijini Baku, lakini inadaiwa Emery ana mpango wa kumtema kwa ajili ya kukisuka upya kikosi chake katika dirisha hili la uhamisho.

Arsenal pia imekuwa ikihusishwa kumchukua beki wa Saint-Etienne, William Saliba, 18, Nicolas Pepe wa Lille, beki wa Roma, Kosta Minolas, na kiungo wa River Plate na Timu ya Taifa ya Argentina, Exequiel Palacios.

# Solskjaer, Unai zakabana usajili EPL

**LONDON, England**



KLABU za Manchester United na Arsenal, baada ya zote kushindwa kumaliza katika nafasi nne bora, katika Ligi Kuu England sasa zinaingia kwenye soko la usajili kwa nguvu.

Makocha wa vikosi hivyo, Ole Gunnar Solskjaer wa huko Old Trafford na Unai Emery wa pale Emirates watakuwa bize kufanya mabadiliko kadhaa kwenye vikosi vyao ili kuja na nguvu mpya kwa msimu ujao.

Kwa wiki sasa United imeripotiwa kujifungia kwenye mazungumzo ya kumnasa Paul Dybala wa Juventus, huku wakipiga hesabu pia za kumnasa kiungo wa Barcelona, Ivan Rakitic ili kuziba pengo la Ander Herrera.

Kocha Ole amekuwa akihusishwa na majina ya mastaa wengine wakiwamo mabeki Harry Maguire, Kalidou Koulibaly na Aaron Wan-Bissaka huku viungo wengine anaowataka ni Dan James, Declan Rice na Gareth Bale.

Kama nyota hao wote watanaswa, basi United ya msimu ujao itakuwa na sura mpya kadhaa kwenye kikosi chake cha kwanza ambapo golini anaweza kuendelea kuwa David De Gea, huku katika nafasi ya ulinzi kutakuwa na Luke Shaw kushoto, Wan-Bissaka kulia na mabeki wa kati ni Maguire na Koulibaly.

Kwenye viungo watatu kutakuwa na Paul Pogba, Rice na Rakitic na upande wa mbele kutakuwa Dybala, kushoto Bale na katikati atakuwa Marcus Rashford.

Kocha Emery, naye bila shaka atakuwa bize kusaka wachezaji anaotaka kuwaongeza kwenye kikosi chake kinachoripotiwa ni huenda kuna mastaa sita wapya wakatua kwenye kikosi chake kwa kuanzia na Juan Mata na Adrien Rabiot anaoweza kuwanasa bure huku akimsaka pia Youri Tielemans na Ryan Fraser wa Bournemouth.

Mipango ya Emery pia ni kumnasa beki wa kati wa Getafe, Djene Dakonam, huku akiwa kwenye nafasi nzuri pia ya kumsajili staa wa Ajax, Hakim Ziyech.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL YAONGOZA KWA MAPATO EPL

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool ilijipatia zaidi ya takribani pauni milioni 152 kutoka kwenye Ligi Kuu England msimu huu ikiwa ni zaidi ya pauni milioni 1.44 dhidi ya mabingwa Manchester City.

City waliingiza kiasi cha pauni milioni 150.9 licha ya kuwa mabingwa lakini walishika nafasi ya pili katika kuingiza mapato.

Liverpool imefanikiwa kupata kiasi hicho cha fedha kutokana na kushiriki katika mechi nyingi zilizorushwa moja kwa moja na televisheni za Uingereza.

Wekundu hao wa dimba la Anfield, ambao walimaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu England wakiwa na jumla ya pointi 97 walionyeshwa wakicheza moja kwa moja mara 29 katika Sky Sports ama BT Sport ikiwa ni mara tatu zaidi ya City.

Aidha kikosi hicho cha City kinachoongozwa na kocha, Pep Guardiola kilipokea pauni milioni 38.4 kwa kumaliza nafasi ya kwanza, ikiwa ni zaidi ya takribani pauni milioni mbili ya fedha zilizopokewa na kikosi cha Jurgen Klopp.

Klabu ya Huddersfield ambayo ilishushwa daraja ilipokea pauni milioni 96.6 baada ya kumaliza wa mwisho.

Klabu zote 20 zilipokea mapato sawa ya pauni milioni 34.4, pamoja na pauni milioni 43.2 kutoka kwenye haki za runinga za kimataifa,kila moja na pauni milioni tano za mauzo.

Mapato ya jumla kwa timu nyingine ni kama ifuatavyo na kwenye mabano kiasi cha fedha nilichoingiza klabu kwa pauni.

Chelsea (146,030,216), Tottenham (145,230,801), Arsenal (142,193,180), Manchester United (142,512,868), Wolves (127,165,114), Everton (128,603,905), Leicester (123,328,078), West Ham (122,528,663), Watford (113,895,527), Crystal Palace (114,215,215), Newcastle (120,130,418), Bournemouth (108,139,973), Burnley (107,340,558), Southampton (104,302,937) Brighton (105,741,728), Cardiff (102,704,107), Fulham (101,904,692) na Huddersfield (96,628,865).

## KWA UFUPI

**RODRIGUEZ AGOMBEWA EPL**

LIVERPOOL, Manchester United na Arsenal, zote zimeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo mchezeshaji wa Colombia, James Rodriguez (27), ambaye hataraji kusaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia Bayern Munich baada ya mkataba wake wa mkopo na Real Madrid kumalizika katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

**SANE ATAKIWA BAYERN**

RAIS wa Bayern Munich, Uli Hoeness amethibitisha kuwa mabingwa hao wa Bundesliga wanataka kumsajili winga wa Manchester City Mjerumani Leroy Sane. ***(Suddeutsche Zeitung - in German)***

**FRASER AKARIBIA ARSENAL**

ARSENAL imesema iko katika mpango wa kumsajili winga, Ryan Fraser (25), baada ya kumalizika kwa Fainali za Ligi ya Europa League, lakini klabu yake ya Bournemouth imeshatangaza dau la nyota huyo raia wa Scotland kuwa ni pauni milioni 30. ***(Independent)***

**MADRID: ASENSIO HAUZWI**

MABOSI wa Tottenham wameanza mazungumza na Real Madrid kwa ajili ya kumsajili kiungo, Marco Asensio (23), lakini tayari vigogo hao wa La Liga wameweka wazi kwamba Mhispania huyo hauzwi. ***(AS - in Spanish)***

**UNITED YAMWANIA RABIOT**

MANCHESTER United bado inahitaji kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot (24), ambaye anajiandaa kuondoka Paris St-Germain kama mchezaji huru katika kipindi cha usajili cha majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

**LIGT AONGEZEWA DAU**

MABOSI wa Manchester United wameamua kuongeza dau hadi kufikia pauni milioni 12 ili kumnasa beki wa kati wa Ajax, Matthijs de Ligt na kwa uamuzi huo wanaamini kwamba watafanikisha mchakato wa kumsajili Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Sport, via Express)***

**BENITEZ AIKACHA ROMA**

KOCHA wa Newcastle United, Rafael Benitez, amewaambia Marseille na Roma kuwa kipaumbele chake ni kukubali kusaini mkataba mpya na klabu yake ya St James' Park baada ya uongozi wa timu hiyo kukubali kutekeleza mahitaji yake aliyowaambia kwa ajili ya msimu ujao. ***(Chronicle)***

**FERNANDES SOKONI**

NEWCASTLE United inajiandaa kumsajili beki wa kulia wa CSKA Moscow, Mbrazil Mario Fernandes aliyezaliwa Urusi ambaye pia anawaniwa na Atletico Madrid ya Hispania. ***(Star)***

**DARMIAN, MATA NJIA MOJA**

NYOTA wanne ambao ni beki Mtaliano Matteo Darmian (29), straika Mbelgiji Romelu Lukaku (26), kiungo Mhispania Juan Mata (31) na mchezaji kutoka Argentina, Marcos Rojo (29) wako njia moja kuondoka katika kikosi cha Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

**INTER YAMWINDA LUKAKU**

INTER Milan imesema iko tayari kuipatia Manchester United kiasi cha pauni milioni 30 pamoja na winga wake raia wa Croatia, Ivan Perisic (30), ili kumnasa straika Mbelgiji Romelu Lukaku. Klabu yake ya zamani wa Everton itapata kiasi cha pauni milioni tano endapo United watamuuza nyota huyo kabla ya mkataba wake haujamalizika. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

**CITY KUMUUZA DELPH**

MANCHESTER City wamesema kuwa wanahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 15 ili kumuuza kiungo wake, Fabian Delph. Klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu England zimeonyesha nia ya kumhitaji nyota huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sun)***

**HOOGEWERF KUTUA UNITED**

MANCHESTER United inatarajia kumsajili mshambuliaji chipukizi, Mholanzi Dillon Hoogewerf (16), baada ya nyota huyo kuondoka katika kituo cha vijana cha timu ya Ajax. ***(Metro)***

## HABARI MICHEZO

# DK. SHEIN ATAKA SHERIA MPYA KULINDA WASANII

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa kitendo cha kuiba kazi za wasanii ni jambo baya na lisilokubalika kwa sababu "wajanja" hao wanajinufaisha wao.

Dk. Shein alisema hayo alipokutana na uongozi wa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo wakati ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa wizara hiyo juzi kwenye Ikulu ndogo iliyoko Kibweni.

Alisema kuwa ni vyema sheria ikatazamwa au ikafanyiwa marekebisho ili jambo hilo lisiendelee kujitokeza na kumaliza dhulma wanazofanyiwa wasanii wakiwamo wasanii wakongwe wa hapa nchini.

Alisema imekuwa ni utamaduni hivi sasa kwa baadhi ya watu kuzitumia kazi za wasanii kwa kujinufaisha wao huku wakiwaacha wahusika wakikosa fedha na kutofaidika na kazi zao huku 'wajanja' hao wakiendelea kujinufaisha.

Alieleza kuwa kuna haja ya kuwekwa mikakati maalum katika kutafuta taratibu na ufumbuzi wa suala hilo kisheria na kutizamwa sheria iliopo hivi sasa kama inakidhi haja juu ya suala hilo ama inahitaji marekebisho.

Aidha, Dk. Shein alieleza ipo haja kwa uongozi wa wizara husika kupitia Idara ya Utamaduni na Sanaa ikalifanyia kazi suala zima la kivazi cha Mzanzibari mwanamke na mwanamume na jinsi kinavyovaliwa.

Pia aliitaka wizara kutizama jinsi ya matumizi na kazi za studio mpya ya kisasa iliyojengwa na Serikali kwa fedha nyingi hapo Rahaleo ambapo iwapo ingelitumika vema ingekuwa mkombozi mkubwa kwa wasanii wa Zanzibar.

Naye Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Lulu Msham Abdalla, alieleza kuwa wizara yake imefanikiwa kuhakikisha kuwa utamaduni, mila na silka za Wazanzibari zinaenziwa, zinaendelezwa kwa manufaa ya Taifa kwa kutumia matamasha, vikundi vya sanaa kufanya maonyesho mbalimbali.

Waziri huyo alisema kuwa wizara hiyo pia imefanikiwa kulinda haki za wasanii na sanaa zao kupitia BASSFU na Ofisi ya Hakimiliki ambapo pia jumla ya matamasha nane yamefanyika, kazi za sanaa 379 zimekaguliwa na mirahaba yenye thamani ya Sh. milioni 105.1 itagaiwa kwa wasanii na wabunifu 1,277.

Alisema kuwa wizara imefanikiwa kukamilisha Sera ya Michezo na imeanza kutumika huku akieleza jinsi walivyofanikiwa kukamilisha matengenezo kwenye viwanja vya Mao-Zedong, Gombani na Amaan.




Kiungo wa Simba, Haruna Niyonzima (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Sevilla FC, Aleix Vidal katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa juzi. Simba ililala mabao 5-4. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Wagombea wawili waondolewa ZFF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAGOMBEA wawili kati ya sita waliojitokeza kuwania Urais katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) ambao unatarajiwa kufanyika Juni 2 mwaka huu wametemwa, imefahamika.

Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Omar Makungu, alisema kuwa wagombea hao wameondolewa katika mchakato huo kwa sababu wameshindwa kukamilisha kujaza fomu kama taratibu zinavyoelekeza.

Makungu aliwataja wagombea hao walioondolewa kuwa ni pamoja na Abdulrahman Mohamed Haji na Haji Ali Salim.

Aliwataja wagombea waliobakia katika nafasi hiyo ni wanne ambao ni pamoja na Khamis Saidi Abdalla, Sefu Kombo Pandu, Ame Abdalla Dunia na Suleiman Mohamed Jabir wakati kwa upande wa Makamu wa Rais waliopita ni Salum Ubwa Nassor, Hussein Ahmada Vuai na Khamis Shaali Choum.

Aliwataja waliopitishwa katika nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya UTendaji ni Salum Ally Haji kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Haji Hassan kutoka Mkoa wa Mjini Magharib pamoja na Faina Idarous Faina, ambaye alikuwa rais wa ZFA. .

Wajumbe wengine kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja ni mchezaji wa zamani wa Miembeni na kocha wa Zimamoto, Sefu Bausi Nassor na Rashid Tamim Khalfan.

Kwa upande wa mikoa miwili ya Pemba wanaowania ujumbe ni Omar Ahmed Awadh (Kaskazini Pemba) na Sefu Mohamed Seif wa Kusini Pemba.

# Mwakyembe afunguka kinachoimaliza michezo

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk.Harrison Mwakyembe amesema kuwa sekta ya michezo bado haijapewa kipaumbele zaidi ili iweze kuleta manufaa katika Taifa.

Mwakyembe alisema hayo katika semina iliyoshirikisha Maafisa Michezo kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini ambayo ilikuwa na lengo la kuinua michezo.

Alisema sekta ya michezo kwa sasa inapaswa kupewa kipaumbele kikubwa na viongozi wanaopaswa kufanya hivyo ni Maafisa Michezo wote kuanzia ngazi ya wilaya, mikoa na kwa kushirikiana na wizara yake.

Alisema kuwa wamefanya semina hiyo ili kuhakikisha malengo ya kuinua michezo yanafikiwa kwa wakati kama zilivyo sekta nyingine ambazo zinafanya vema huku pia akisema michezo ni biashara kubwa duniani ndio maana tunashuhudia wachezaji wa Ulaya wanaishi maisha mazuri .

**Kutokana na hilo alisema maafisa michezo wanapaswa kuchangamka kuinua vipaji vya wachezaji chipukizi ili waweze kufika mbali katika maisha yao ya kila siku.**

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga, alisema semina hiyo ni maalumu kwa kila ofisa michezo kutoa changamoto na ushauri kwa ajili ya kuendeleza na kuinua michezo.

Tenga alisema hakuna sababu ya kurudi nyuma na kinachotakiwa ni kuendelea kujituma na kuona kila mchezo unasonga mbele kwa kuhakikisha wachezaji wanaandaliwa kwa wakati.

Naye Dk. Jonas Tiboroha ambaye ni Ofisa Michezo wa Wilaya ya Ubungo, alisema watawasilisha dokezo kwa waziri ndani ya siku mbili ili kuona nini kifanyike kwa ajili ya kuinua michezo. Tiboroha alisema mabadiliko machache katika utawala wa wilaya na mikoa kwenye michezo yakifanywa kwa weledi, basi kila kitu kitakwenda sawa katika sekta hiyo.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.SIMBA | 36 | 29 | 4 | 3 | 76 | 14 | 91 |
| 2.YANGA | 37 | 27 | 5 | 5 | 57 | 25 | 86 |
| 3.AZAM | 37 | 20 | 12 | 5 | 52 | 21 | 72 |
| 4.KINONDONI MC | 37 | 12 | 16 | 9 | 38 | 25 | 52 |
| 5.MTIBWA SUGAR | 37 | 14 | 7 | 16 | 36 | 34 | 49 |
| 6.LIPULI | 37 | 12 | 13 | 11 | 31 | 37 | 49 |
| 7.MBEYA CITY | 37 | 13 | 8 | 16 | 38 | 40 | 47 |
| 8 COASTAL UNION | 37 | 11 | 14 | 12 | 32 | 42 | 47 |
| 9.NDANDA | 37 | 12 | 12 | 13 | 24 | 34 | 48 |
| 10.SINGIDA UNITED | 37 | 11 | 12 | 14 | 30 | 39 | 45 |
| 11.STAND UNITED | 36 | 12 | 8 | 16 | 36 | 45 | 44 |
| 12 ALLIANCE | 36 | 11 | 11 | 14 | 30 | 39 | 44 |
| 13.MBAO | 37 | 11 | 11 | 16 | 26 | 40 | 44 |
| 14.TZ PRISONS | 37 | 10 | 13 | 14 | 27 | 30 | 43 |
| 15.BIASHARA UNITED | 36 | 11 | 10 | 15 | 29 | 34 | 43 |
| 16.KAGERA SUGAR | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 17.RUVU SHOOTING | 37 | 10 | 12 | 15 | 34 | 43 | 42 |
| 18.MWADUI | 37 | 10 | 8 | 18 | 44 | 53 | 41 |
| 19.JKT TANZANIA | 36 | 9 | 14 | 13 | 24 | 34 | 41 |
| 20.AFRICAN LYON | 37 | 4 | 11 | 22 | 23 | 51 | 23 |

Michezo

Jumamosi Mei 25, 2019

Nipashe



Liverpool yaongoza kwa mapato EPL

HABARI UK 30



Beki wa Simba, Mohammed Hussein (kulia), akijaribu kumtoka mchezaji wa Sevilla katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa juzi jijini Dar es Salaam. Simba ilifungwa mabao 5-4. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# SEVILLA: SIMBA NI HATARI

## Kiwango chawashangaza, Lugola kuwakabidhi kombe la ubingwa leo...

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya kukubali kufungwa na mabingwa mara tano wa Ligi ya Europa, Sevilla FC, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wamepongezwa kutokana na kiwango walichokionyesha katika mchezo huo wa kirafiki uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Sevilla FC ikitokea nyuma ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 5-4, ziara yao ya kuja hapa nchini ilidhaminiwa na Kampuni ya Kubahatisha ya SportPesa Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo kumalizika, Kocha wa Sevilla, Joaquin Caparros, alisema kuwa wapinzani wao walikuwa bora zaidi katika kipindi cha kwanza na hali hiyo ilimfanya awaambie wachezaji wake wapambane na kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo.

Caparros alisema kuwa awali hakufahamu kama Tanzania na Afrika Mashariki kuna timu ya kiwango hicho na kwa changamoto waliyoipata wachezaji wake, amewapongeza nyota wa Simba kwa ushindani waliouonyesha katika mchezo huo.

"Soka ni mchezo wa heshima, tunaiheshimu Simba, ni mabingwa wa Ligi Kuu, kwa sababu hiyo ndiyo maana mchezo huu umekuwa mgumu sana, ulikuwa ni mchezo wa kirafiki tu, kudumisha uhusiano wa Ligi ya Hispania Laliga na timu za Ukanda wa Afrika Mashariki kupitia SportPesa. Pamoja na kuwapa burudani mashabiki, kwa wachezaji mchezo wa aina hii ni fursa kwao kujiuza," aliongeza kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema kuwa kitendo cha timu yake kupata nafasi ya kuwafunga Sevilla mabao manne ni jambo la kujivunia kwa sababu wameonyesha kwamba wanaweza.

Aussems alisema kuwa hakufurahishwa na matokeo ya mwisho ya mechi hiyo, kwa sababu alidhamiria kufanya mabadiliko katika kikosi chake ili wachezaji wake wengi wapate nafasi ya kuweka historia na kucheza na timu hiyo kubwa.

"Nilifanya mabadiliko ili kila mchezaji apate nafasi ya kucheza na moja ya timu kubwa Ulaya, lakini baada ya mabadiliko mambo yalibadilika. Kuifunga Sevilla magoli manne ni jambo kubwa sana na najua hata wao hawakutegemea," alisema Mbelgiji huyo ambaye amesaini mkataba mwingine mpya wa miaka miwili wa kuendelea kuitumikia Simba. Kiungo Mnyarwanda Haruna Niyonzima, alisema kuwa kila mchezaji wa Simba alitamani kucheza na timu hiyo yenye hadhi ya kimataifa na katika kutimiza ndoto hizo, timu yao ilipoteza mechi hiyo licha ya kuongoza kwa muda mrefu.

**LUGOLA KUKABIDHI KOMBE**

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, anatarajia kuwa mgeni rasmi na kuwakabidhi kikombe cha ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu baada ya kumalizika kwa mchezo wa ligi hiyo kati ya Simba dhidi ya Biashara United utakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Msemaji wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa mechi hiyo itaanza saa 9: 00 mchana na baada ya hapo mabingwa hao watapita katika mitaa mbalimbali jijini ili kutoa nafasi kwa mashabiki wao kuwashangilia wachezaji wa timu hiyo ambao msimu huu pia walifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha Mkuu wa Biashara United, Amri Said, alisema kuwa anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu sana kwa sababu wao wanahitaji kujinasua kwenye janga la kushuka daraja wakati Simba inahitaji kumaliza msimu huu kwa heshima.

# Mo awazidi akili Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

NDOTO za Yanga kufanikiwa kunasa saini ya kiungo wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Jonas Mkude huenda "zimeyeyuka" baada ya bosi mkuu wa klabu hiyo yenye makao yake makuu Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam, kuweka wazi mambo yako vema na mchezaji huyo.

Mkataba wa Mkude na Simba umemalizika na nyota huyo anahusishwa na mipango ya kujiunga na Yanga baada ya klabu yake kuonyesha kutokuwa tayari kutoa kiasi cha fedha alichohitaji.

Taarifa za ndani kutoka Simba zilidai kuwa Mkude, mchezaji ambaye ana zaidi ya miaka 10 katika klabu hiyo akitokea Simba B, kiungo huyo anataka alipwe kiasi cha Sh. milioni 120.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed Dewji 'Mo' aliwataka mashabiki wa klabu hiyo kutokuwa na wasiwasi wowote juu ya kiungo wao huyo.

Hata hivyo Mo hakuwa tayari kuweka wazi kama tayari ameshamalizana na Mkude kama ambavyo amekuwa akifanya kila anapokamilisha mchakato wa kumpa mkataba mpya mchezaji anayeongeza au yule anayesajiliwa kwa mara ya kwanza.

"Wana-Simba msiwe na wasiwasi, Mkude haendi kokote, Jumaa Kareem," alisema mfanyabiashara huyo.

Mo amelazimika kutoka kauli hiyo ili kuwatuliza Simba ambao msimu uliopita walishuhudia mshambuliaji wao, Ibrahim Ajibu akienda Yanga kama mchezaji huru.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >